




**Kinamama** waweka kope bandia, lenzi hatarini kwa upofu

UKURASA 4




UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Agosti 31, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581419

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ | The Nipashe Digital | nipasheTZ | nipashedigital | epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com | 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




MABADILIKO YA SAMIA

# Kilichojificha uteuzi Naibu Waziri Mkuu

UKURASA 2 & 3

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### SOMO LA BIASHARA KUWA LAZIMA SEKONDARI



BUNGE limeelezwa kuwa katika mitaala mipya ya elimu somo la Biashara limepangwa lazima kwa wanafunzi wote kuanzia...

UKURASA WA 19

### RAIS ALI BONGO APINDULIWA, KIZUIZINI



VIONGOZI wa kijeshi Gabon wametangaza kuchukuwa madaraka, siku chache baada ya taifa hilo, kufanya uchaguzi na kumrejesha..

KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

## Mkuu Upelelezi ashangaa Wakili Kibatala kuwa na nyaraka za siri za jeshi


UKURASA 5



Naibu Waziri Mkuu, pia Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa



Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Dunstan Kitandula

## WALIOTEMWA



Aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula



Aliyekuwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Atupele Mwakibete



Aliyekuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja

MICHEZO MAKALI YA YANGA NI KIPINDI CHA PILI UK.24 KATUNI UK.6

# Kilichojificha uteuzi Naibu Waziri Mkuu


Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa


Waziri wa Madini, Anthony Mavunde


Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa


Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amefanya mabadiliko madogo ya Baraza la Mawaziri na makatibu na naibu makatibu wakuu huku wadau wakitoa maoni kuhusu siri iliyojificha katika uteuzi Naibu Waziri Mkuu.

Katika mabadiliko aliyoyafanya, Rais Samia ameanzisha nafasi ya Naibu Waziri Mkuu kwa kumteua Dk. Dotto Biteko ambaye pia anakuwa Waziri wa Nishati. Kabla ya uteuzi huo, alikuwa Waziri wa Madini na kwa wadhifa mpya atakuwa anashughulikia uratibu wa shughuli za serikali.

Biteko anakuwa mtu wa tatu kushika wadhifa huo. Waliowahi kushika na miaka kwenye mabano ni Dk. Salim Ahmed Salim (1985-1989), na Augustine Mrema (1992-1994).

Rais amefanya uteuzi huo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 36(1) inayosema: 'Bila ya kuathiri masharti mengineyo yaliyomo katika Katiba hii na ya sheria nyingine yoyote, Rais atakuwa na mamlaka ya kuanzisha na kufuta nafasi za madaraka ya namna mbalimbali katika utumishi wa serikali ya Jamhuri ya Muungano."

### MAONI YA WADAU

Kutokana na mabadiliko hayo, wachambuizi wa siasa, wasomi na wanasiasa. Wametoa maoni huku wakisema ni hatua nzuri ya kujenga serikali imara baada ya kuona kuna upungufu mahali.

Mchambuzi wa masuala ya siasa, Abdulkarim Akiki, alisema hatua ya Rais kumteua Naibu Waziri Mkuu ina lengo la kuongeza nguvu ya kiutendaji serikalini. Alisema Rais amerudisha nafasi hiyo ili kumsaidia Waziri Mkuu kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli serikali.

Mhadhiri Msaidizi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Nassor Kitunda, alisema nafasi ya naibu waziri mkuu itaongeza nguvu ya kiutendaji katika Baraza la Mawaziri kutokana na Waziri Mkuu kuwa na majukumu makubwa, hivyo anahitaji mtu wa kumsaidia baadhi ya mambo.

Alisema kuwapo kwa nafasi hiyo wakati mwingine ni ubunifu wa kiongozi aliyeko madarakani ili kufikia malengo aliyojiwekea kama vile Rais alivyoamua kutenganisha wizara za ujenzi na uchukuzi kwa kuwa ameona kila moja inahitaji usimamizi wa karibu.

Kuhusu kubadili mawaziri na makatibu wakuu alisema rais anao wajibu wa kuchagua watu ambao anaona atafanya nao kazi vizuri na kuondoa malalamiko ya wananchi juu ya utendaji kazi katika wizara husika.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Mstaafu, Ludovick Utouh, alisema mabadiliko hayo yana nia njema ya kuongeza ufanisi katika shughuli za serikali na Rais ana mamalaka kikatiba kufanya uamuzi huo pale anapoona kuna kasoro za kiutendaji.

Alisema anaamini alichokifanya Rais Samia amekitafakari na kumekuwa na majadiliano na watu wanaomshauri, hivyo Watanzania waamini kuwa mabadiliko hayo yanalenga kuboresha utendaji kazi katika serikali.

Otouh alisema si mara ya kwanza mabadiliko kama hayo kufanyika kwa kuwa Rais wa awamu ya tano, Hayati John Magufuli, aliitengenisha iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini na zikawa wizara mbili hali iliyochangia kuongeza ufanisi katika Wizara ya Madini.

Mshauri Mwelekezi na mchambuzi wa Siasa, Luwaga Kizoka, alisema mabadiliko hayo yanalenga kuongeza ufanisi wa utendaji kazi serikalini na hatimaye kuleta matokeo mazuri.

Alisema kitendo cha Januari Makamba kupelekwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kitaongeza ufanisi wa utendaji kazi kwa kuwa ni eneo ambalo amefanya kazi kwa muda mrefu, hivyo analifahamu vizuri.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sera za Kimataifa Afrika, Omary Mjenga, alisema Rais ana mamlaka ya kufanya mabadiliko anavyotaka ili kuboresha utendaji na anaongozwa na Katiba ya nchi.

Alisema uamuzi wa kutenganisha wizara ya ujenzi na uchukuzi ni uamuzi wa busara kwa kuwa uchukuzi na ujenzi ni maeneo mapana yanayohitaji kufanyiwa kazi kiutofauti ili kuleta ufanisi.

Ofisa Tawala, Ofisi ya Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Taaluma), Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Dickson Kikoti, alisema alichokifanya Rais ni jambo la kawaida na ana mamlaka ya kufanya hivyo pale anapoona kuwa anahitaji kuboresha ufanisi wa kazi kwa viongozi ambao ndio wasaidizi wake.

### MABADILIKO

Katika mabadiliko hayo madogo, Rais ameivunja Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na kuunda wizara mbili ambazo ni Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Uchukuzi.

Aidha, kwenye mabadiliko hayo, aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula; Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, wameachwa.

Pia alisema Rais Samia ameimarisha Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kuongeza nafasi ya Naibu Waziri na Katibu Mkuu watakaoshughulikia masuala ya Afrika Mashariki.

Mawaziri wapya na wizara kwenye mabano ni Jerry Silaa (Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi) na Anthony Mavunde (Madini) na Prof. Makame Mbarawa amehamishwa kutoka Ujenzi na Uchukuzi kwenda Uchukuzi. January Makamba amehamishwa kutoka Nishati kwnda Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Innocent Bashungwa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwenda Ujenzi

Dk. Stergomena Tax kutoka Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Kwenda Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Damas Ndumbaro kutoka Katiba na Sheria kwenda Utamaduni, Sanaa na Michezo na Balozi Dk. Pindi Chana kutoka Utamaduni, Sanaa na Michezo kwenda Katiba na Sheria. Wengine ni Mohamed Mchengerwa kutoka Maliasili na Utalii kwenda Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serilaki za Mitaa (TAMISEMI) na Angellah Kairuki kutoka TAMISEMI kwenda Maliasili na Utalii.

Naibu Mawaziri waliohamishwa ni Godfrey Kasekenya kutoka Ujenzi na Uchukuzi Kwenda Ujenzi, David Silinde kutoka Mifugo na Uvuvi Kwenda Kilimo, Stephen Byabato Nishati Kwenda Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki akishughulikia masuala ya Afrika Mashariki.

Wapya walioteuliwa kuwa naibu mawaziri na wizara kwenye mabano ni Alexander Mnyeti (Mifugo na Uvuvi). David Kihenzile (Uchukuzi), Judith Kapinga (Nishati) na Dunstan Kitandula (Maliasili na Utalii).

### MAKATIBU WAKUU

Katika Uteuzi wa Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, Rais Samia amemteua Prof. Godius Kahyarara aliyekuwa Katibu Tawala Mkoa wa Geita kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi na Mhandisi Cyprian Luhemeja aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji amekuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu).

Balozi Prof. Kennedy Gastorn ameteuliwa kuwa Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki.

***• Imeandikwa na Jennipher Gilla na Emmaloveness Gaston (DAR) na Augusta Njoji, DODOMA.***

## Dk. Mpango ataka utafiti zaidi kuongeza makusanyo ya kodi Afrika

**Na Restuta James**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ametoa rai kuongeza nguvu katika utafiti, ili kupata njia mwafaka ya kuongeza makusanyo ya serikali za Afrika.

Dk. Mpango alitoa rai hiyo jijini Dar es Salaam juzi, kupitia hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alipofungua Mkutano wa Nane wa Jukwaa la Kodi Afrika (ATAF).

Alisema utafiti unapaswa kufanyika kwa kushirikisha taasisi mbalimbali, ili kuunda mfumo wa kisasa utakaogusa maeneo mengi yanayoweza kuipatia serikali mapato.

Mkutano huo ambao mwenyeji wake ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), umewakutanisha wataalamu zaidi ya 300 kutoka nchi 43 barani Afrika, ukiwa na kaulimbiu ya 'Masuala ya Kikodi Yanayojiri.'

Pamoja na mambo mengine, mkutano huo utajadili ripoti 43 za utafiti wa kikodi kati ya 150 zilizowasilishwa. Lengo ni kutoa mapendekezo ya maeneo mapya ya kikodi zikiwamo sekta za gesi, mafuta, madini, mazingira na biashara za kiteknolojia.

"Pamoja na jitihada mbalimbali zinazoendelea kufanywa na nchi zetu, bado kuna changamoto ya ukusanyaji mapato kutokana na ukubwa wa sekta isiyo rasmi… takwimu za mwaka 2021 zinaonyesha kwamba mchango wa kodi katika Pato la Taifa ni asilimia 14.55," alisema.

Alizishauri mamlaka za mapato kutunga sera nzuri zitakazovutia ulipaji kodi wa hiari na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika utendaji kazi.

"Ushirikiano kati ya watafiti, watunga sera na watendaji katika mamlaka za kodi utaunganisha nguvu zitakazoipatia serikali mapato ya kutosha kuwekeza katika sekta muhimu za afya, elimu na miundombinu. Utatusaidia kuweka mifumo rahisi inayotekelezeka," alisema.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema Afrika imebarikiwa kuwa na maliasili nyingi ambazo zinaweza kutatua changamoto za kiuchumi na kujiletea maendeleo.

Alisema wizara yake iko tayari kuongeza nguvu katika eneo la utafiti ili kutunga sera nzuri za kikodi zinazoendana na mazingira yaliyopo.

Alisema Afrika ni bara lenye uchumi unaokua kwa kasi unaoongeza watu wenye mapato makubwa, hivyo ni muda mwafaka kuwa na njia nzuri ya kuwatoza kodi.

Katibu Mtendaji wa ATAF, Logan Wort, alisema lengo la jukwaa hilo ni kufanya utafiti na kutoa njia bora za kuongeza wigo wa makusanyo ya serikali.

Alisema takwimu zinaonyesha Bara la Afrika linapoteza zaidi ya dola za Marekani bilioni 88 kutokana na kushindwa kukusanya kodi.

HABARI KITAIFA

# ...wabunge wapongeza, wasema yamechelewa

**Na Romana Mallya,** DODOMA



Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa

WABUNGE wamepongeza mabadiliko katika Baraza la Mawaziri yaliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan jana, baadhi yao wakidai kiongozi huyo alichelewa kuyafanya.

Mbunge wa Sengerema, Hamisi Tabasamu, alisema mabadiliko hayo waliyategemea japo yamefanywa kwa kuchelewa.

"Mfano, katika nishati mabadiliko haya yanaweza kuleta mapinduzi makubwa kwa sababu waagizaji wa mafuta ya rejareja na wananchi kwa uhaba huu mkubwa wa mafuta, ni jambo lililotegemewa kunahitajika mabadiliko makubwa.

"Nishati ya umeme Mama (Rais Samia Suluhu Hassan) tunamshukuru kwa kugawa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, huu ni ushauri tuliotoa bungeni mwaka jana kwamba, kwa miradi iliyopo katika sekta ya Uchukuzi ilikuwa ni lazima isimamiwe na mawaziri wawili wenye dhamana ili kupata ufanisi katika kazi, bado katika Nishati tulitaka tupate waziri pia, wa nishati ya umeme na waziri wa nishati wa mafuta na gesi," alisema.

Tabasamu alisema wanamshukuru Rais, sasa wataanza kuona namna gani wanatakiwa kufanya kazi ambayo anaitaka.

Akizungumzia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, alimpongeza Rais kwa kufanya mabadiliko kwa sababu ilikuwa imelala na sasa amepata waziri kijana, Jerry Silaa, wanaamini atafanya kazi na kuleta mapinduzi makubwa.

"Uteuzi wa Manaibu waziri, mfano mtu kama Alexander Mnyeti haya ni mabadiliko makubwa, tunamshukuru Rais kwa kutuletea vijana ambao wataanza na kazi kubwa. Hizi wizara ambazo hazijafanyiwa mabadiliko nao wasijisahau kwa sababu mama anaendelea na haya mabadiliko," alisema.

Mbunge wa Jimbo la Konde Pemba Kaskazini, Mohamed Said Issa, alisema Rais Samia amewaaminisha wananchi kwamba wakati wowote nafasi ya uwaziri siyo ya kujiamini ni nafasi ya kiutendaji na pale atakapoona anataka kubadilisha atafanya hivyo.

"Hapa nchini kuna shida ya baadhi ya mambo, mfano nishati ya mafuta, shida ya dola kwa hiyo Mheshimiwa Rais ninahisi mabadiliko haya yametokana na kadhia ambayo wananchi wanazipata lengo lake ni kutaka kubadilisha kuona kwamba tunakwenda kwa kasi haya matatizo ambayo yapo ili yapate mwarobaini wake," alisema.

Alisema mabadiliko hayo ambayo ndani yake ipo damu changa (vijana) anaamini kutakuwa na mabadiliko.

"Kwenye nishati kumefanyika mabadiliko, hali iliyokuwapo ya kiutawala ndiyo ilikuwa inaleta usumbufu, kufanya hivyo mimi kama mwakilishi mbunge wa jimbo nimeliona hili litaleta mabadiliko chanya," alisema.

Kuhusu nafasi mpya ya Naibu Waziri Mkuu, Dotto Biteko, alisema wamekuwa wakimwona Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizunguka nchi nzima, kwa uteuzi huo atakwenda kumsaidia kazi.

"Unaona Mheshimiwa Dotto Biteko alipokuwa peke yake Wizara ya Madini kazi aliyofanya ilikuwa inachangia asilimia nane Pato la Taifa na muda si mchache alitaka kuipeleka kwenye asilimia 10, ninaona atatupeleka pazuri kama taifa," alisema.

Mbunge wa Namtumbo, Victor Kawawa, alisema uamuzi wa Rais ambao umegusa kundi la vijana anaamini utaleta mabadiliko kwa sababu hata Bunge hili vijana ni wengi.

"Kwa hiyo ni wakati wao vijana mwanzo walikuwa wanapata uzoefu wa shughuli za Bunge na shughuli za serikali na sasa wameshakomaa kama siyo kamili, lakini watakuwa wamefika mbali kukomaa.

"Ni wakati wao tunaamini watatusaidia nchi yetu, huu ni utaratibu wa serikali wa kawaida unavyokwenda wa baraza ukiona mahali kama timu ya mpira mahali pana pwaya au mwendokasi wako unabadilisha wachezaji na lazima uweke mwenye nguvu na mwendokasi," alisema.

Alisema mategemeo yao ni kwenda kuongeza kasi na kuwavusha katika Uchaguzi Mkuu ujao.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mjini Unguja, Asha Abdallah Juma 'Mshuwa' alisema, wamepokea kwa mikono miwili mabadiliko hayo kwa kuwa yameleta nafasi mpya, Biteko anayekwenda kumsaidia Waziri Mkuu, ili kupata mafanikio ya haraka.

"Uteuzi wa vijana mfano Jerry Silaa ni kijana mwenye uwezo na ana tabia nzuri ili uwe kiongozi ni lazima uwe na sifa hizi, na siyo uelezeki wala huambiliki. Kwenye ardhi tunajua kuna malalamiko kadhaa ambayo wananchi wanalalamikia, tukipata mtu anayesikiliza watu tunaamini yataumbuka.

"Kuhusu uteuzi wa Judith Kapinga, anaonyesha umahiri namna anavyoshughulikia vijana na kutoa michango yake inayoendana na mambo ya kisheria humu bungeni. Inaonyesha namna Rais Samia anavyowasogeza vijana ili wajiweke tayari katika kushika nchi siku za mbele," alisema.

Kuhusu uteuzi wa Alexander Mnyeti, alisema ni mtu mwenye uwezo na kutaka wasaidiane na mawaziri hao ili waweze kufanya kazi zao kwa umakini na nguvu zaidi kwa kuwa mabadiliko ni lazima na kuwataka walioachwa wasisikie unyonge.

"Mimi mwenyewe niliwahi kuwa waziri nina utamani, lakini miaka 20 sasa sijarudishwa tena. Ninampongeza Rais Samia kwa mabadiliko haya aliyofanya leo mtu asije kujisahau na kuona nimeshashika nafasi imeshakuwa yangu, siyo yake nafasi ni utumishi uliotukuka wawatumikie Watanzania kwa kumsaidia Rais Samia kuiongoza nchi iweze kupaa.

Kuhusu uteuzi wa January Makamba kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, alisema ni kijana mwenye uwezo hasa nyanda za kimataifa.

"Tumewahi kwenda naye ziara wakati wa awamu ya Rais Kikwete, tulipokwenda kumtembelea Rais Barrack Obama, Marekani, January alifanya kazi kubwa, kwa hiyo atasaidia kuitangaza Tanzania na kuunganisha uhusiano wa kimataifa kwa nchi mbalimbali na nchi kujijenga kibalozi, kidiplomasia na kiuchumi,' alisema.

# Somo la Biashara kuwa lazima sekondari

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa katika mitaala mipya ya elimu somo la Biashara limepangwa lazima kwa wanafunzi wote kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne kwa mikondo yote miwili ya elimu ya jumla na elimu ya amali.



Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga (pichani) aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Zainabu Katimba.

Mbunge huyo alihoji lini serikali itaboresha mitaala ya elimu ili mafunzo ya biashara yatolewe kuanzia shule za msingi.

Kipanga akijibu swali hilo alisema wizara ipo katika hatua za ukamilishaji wa mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 na mitaala katika ngazi ya elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Mafunzo ya Ualimu.

Aidha, alisema wizara imevielekeza vyuo vikuu kuhusisha na kufanya maboresho ya mitaala yote ili iendane na dira na mipango ya maendeleo ya taifa katika kutoa elimu itakayompa kijana wa Kitanzania ujuzi.

"Wizara inatambua umuhimu wa somo la biashara na hivyo somo hili limepangwa kuwa la lazima kwa wanafunzi wote kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne kwa mikondo yote miwili ya elimu ya jumla na elimu ya amali."

"Aidha, kwa ngazi ya elimu ya msingi darasa la I-VI mitaala imetilia mkazo elimu ya fedha pamoja na elimu ya ujasiriamali ambapo elimu ya fedha imechopekwa kwenye somo la Hisabati na Elimu ya Ujasiriamali imechopekwa kwenye somo la Sanaa na Michezo, lugha, Jiografia na Mazingira," alisema.

Alieleza kuwa vyuo vikuu vya serikali na binafsi kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) vimepata mafunzo mbalimbali ya kuandaa programu zinazoendana na vipaumbele vya nchi na mahitaji ya soko la ajira.

Kupitia utaratibu huo, alisema zaidi ya programu 300 zitaanzishwa au kuhusishwa ikiwamo somo la biashara ili kuendana na mahitaji ya sasa ya kijamii, kiuchumi na soko la ajira.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
WAKALA YA BARABARA TANZANIA

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Wakala ya Barabara TANROADS-Ruvuma inautangazia umma kuwa itaondosha vifaa chakavu kwa njia ya mnada kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini.

| | |
|---|---|
| Tarehe ya Mnada | 20 Septemba 2023 |
| Muda wa Mnada | Kuanzia saa 4 asubuhi |
| Eneo la Mnada | • Kambi ya Ujenzi Madaba<br>• Kambi ya Ujenzi Lilondo<br>• Ofisi ya Meneja Mfaranyaki, Songea mjini |
| Vifaa vitakavyonadiwa | • Samani mbalimbali za ofisi<br>• Magari na majenereta. |
| Wanaoruhusiwa kushiriki Mnada | Umma wote |
| Tarehe za ukaguzi wa bidhaa | 17-19 Septemba 2023, kuanzia saa 4-8 mchana katika maeneo husika |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Vifaa vitauzwa jinsi vilivyo mahali vilipo.
2. Mnunuzi atapaswa kulipa 25% ya mali ponakukamilisha 75% ya malipo katika kipindi kisichozidisiku 14. Mnunuzi akishindwa kufanya hivyo atapoteza haki za umiliki na amana yake.
3. Mnunuzi atakayetaja bei na kushindwa kulipa 25% ya malipo atahesabiwa kuwa mvuruga mnada na hatua zitachukuliwa dhidi yake kwa mujibuwa Sheria.
4. Gharama zote za ukaguzi, uondoshaji wa mali na uhamishaji umiliki (ikiwemo kushughulikia kadi kwa vyombo vya moto) zitakuwa juu ya mnunuzi na atapaswa kuondoa mali husika ndani ya siku 7 baada ya malipo kukamilika.
5. Kodi zote na gharama nyinginezo zitagharimiwa na mnunuzi.
6. Malipo yote yatafanyika kwa mfumo wa Serikali kwa kutumia *Control Number.*
7. Tangazo pia linapatikana katika tovuti ya TANROADS na ofisi ya mkoa Ruvuma.

Wakala ya Barabara
Ofisi ya Meneja wa Mkoa–Ruvuma
Simu: + 255 25 2602179/2600425
Baruapepe: rm-ruvuma@tanroads.go.tz.

217578202

# Kinamama wanaoweka kope bandia, lenzi hatarini

**Na Joseph Mwendapole**

HOSPITALI ya CCBRT imetahadharisha kuwa wanawake wanaoweka kope bandia na wanaovaa lenzi za miwani bila kupima kuwa wako hatarini kupata matatizo makubwa ya kuona kiasi cha kuhitaji upasuaji.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Dk. Cyprian Tomoka, alisema hayo jana wakati akizungumza na wahariri na waandishi wa habari waliotembelea hospitali jana kuangalia huduma zinazotolewa na taasisi hiyo.

Alisema madaktari wanashauri mtu yeyote akitaka kuweka kifaa chochote kwenye mwili wake afanye vipimo vya awali ili kujua kama anachotaka kuweka kitaendana na mwili wake au la ili kuepuka matatizo ambayo yamewapata watu wengi.

Dk. Tomoka alisema hivi sasa imekuwa kawaida kwa watu kununua miwani holela na wengine kubandika kope jambo ambalo limeongeza idadi ya watu wenye shida ya macho wanaokwenda kupata tiba katika hospitali hiyo.

"Hata ukitaka kuweka lenzi ya kuonea au kope basi pima afya ya macho yako ijulikane kwa sababu tunapata wagonjwa ambao wanakuja kutibiwa macho yenye viashiria kwamba huyu aliweka kope bandia na huyu aliweka lenzi ya kuonea na mwingine anakuwa na vidonda machoni ingawa hawasemi sababu," alisema.

Alisema kila siku hospitali hiyo imekuwa ikipokea wagonjwa wenye shida ya macho ambao umesababishwa na wahusika kuvaa kope bandia au lenzi za miwani bila kupima afya ya macho.

Pia alisema kwa wagonjwa wanaochelewa kwenda hospitalini na kwenda wakiwa tayari na vidonda kwenye macho wanakuwa kwenye hatari kubwa ya kupoteza uoni moja kwa moja.

Alisema baadhi ya watu wamekuwa na mtazamo kwamba CCBRT inatibu macho na kurekebisha viungo pekee wakati inatoa huduma zote zikiwamo za mama na mtoto, uchujaji wa damu (dialysis), mifupa, nyonga, magoti.

"Kwa siku za karibuni kumekuwa na changamoto ya magonjwa ya figo kwa hiyo tumeamua kuanzisha kitengo cha kuchuja figo na tumeanzisha kitengo cha watu wenye utindio wa ubongo kwa kuwapa huduma mbalimbali saidizi za kuwaweka sawa," alisema.

Kuhusu ugonjwa wa fistula kwa wanaume, Dk. Tomoka alisema ugonjwa huo huwa unawapata baada ya kupata ajali na kuathiri njia ya mkojo, hivyo kusababisha mkojo kupita njia isiyo yake.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Adinani Mpyagila akihutubia mkutano wa hadhara uliojadili masuala mbalimbali ya maendeleo pamoja na kutoa elimu kuhusu uwekezaji kwenye bandari, katika kijiji cha Naipanga, hivi karibuni. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Tanzania kuongeza uzalishaji mpunga

**Na Renatha Msungu**

SERIKALI imesema ushirikiano inaofanya na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) na mashirika ya kimataifa, utachochea uzalishaji wa mpunga nchini.

Akifungua mkutano wa siku tatu wa wadau wa zao la mpunga kutoka nchi 11 jijini Dar es Salaam juzi, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli, alisema washiriki wa uzalishaji mpunga wataleta mkakati wa kuboresha uzalishaji wa zao hilo kwa nchi za Afrika Mashariki na Kusini.

Alisema Tanzania itakuwa na nguvu kubwa katika kuendeleza zao la mpunga kama mazao muhimu. Ushirikiano wa wakulima na taasisi za utafiti, hasa TARI na mashirika ya kimataifa umekuwa kichocheo kikubwa.

"Tanzania kwenye takwimu inashika nafasi ya pili Afrika kwa kuzalisha mpunga ikiongozwa na Madagascar, hivyo Taasisi ya Utafiti wa Mpunga Kimataifa (IRRI) imeona Tanzania ina eneo lenye rutuba, hivyo ardhi yake inafaa kwa kuzalisha mpunga zaidi," alisema Mweli.

Aliongeza kuwa mpunga ni chakula na ni biashara. Soko lake la ndani na nje ni kubwa, hivyo uzalishaji unapaswa kuongezeka ili kufikia lengo.

"Serikali inapigania mabadiliko katika matumizi ya mpunga kwa kutumia teknolojia ya kilimo ili kuongeza uzalishaji wa mpunga kutoka chini ya tani 2.5 kwa hekta hadi tani tano au zaidi ifikapo mwaka 2030," alisema.

Katibu Mkuu alisema lengo la serikali ni kuzalisha mpunga wa kutosha kukidhi mahitaji ya kitaifa kuchangia katika usalama wa chakula Afrika na kuwa mzalishaji namba moja wa mpunga barani.

Alisema kwa programu ya RBI ni ushirikiano wa sekta muhimu na binafsi uliolenga kula na kutumia aina bora za mpunga kwa wakulima wadogo katika Afrika Mashariki na Kusini.

Mweli alisema Tanzania ina jukumu kubwa kama mzalishaji mkuu wa mpunga na mipango inatekelezwa na IRRI.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dk. Geoffrey Mkumilo alisema katika mkutano huo wanatarajia kuja na mikakati mikubwa kwa nchi kwa kuwa ardhi yake inafaa kwa kilimo cha umwagiliaji na mvua.

"Tanzania ni mojawapo ya wazalishaji wakuu wa mpunga Afrika, lakini kuna nafasi kubwa ya kuboresha kiwango chetu cha wastani wa tani 2.5 kwa hekta. Ni eneo ambalo linahitaji umakini wa kitaifa, kikanda na kibara," alisema Dk. Mkumilo.

Mwakilishi wa Kikanda wa IRRI Afrika, Dk. Abdelbagi Ismail, alisema Tanzania na nchi nyingi za Afrika Mashariki na Kusini zinachochea maboresho katika uzalishaji wa mpunga ili kupambana na njaa na umaskini wa kipato kwa mamilioni ya wakulima wadogo.

Alisema mpunga ni chakula, pia ni biashara, hivyo wana jukumu la pamoja kubuni na kuongeza uzalishaji wake na kuwa endelevu.

"Ninaamini kwa pamoja tunaweza kutimiza mengi zaidi na kuleta tofauti ambayo hakuna mmoja wetu angeweza kufanya pekee yake tuendelee na ushirikiano huu mzuri," alisema Dk. Ismail.

# Profesa Bisanda: Mabadiliko ya mitaala chachu ya maendeleo

**Na Miraji Msala**

MABADILIKO katika jamii ni kitu ambacho kinatokea kila siku na hivyo mabadiliko ya mitaala ya elimu nchini ni muhimu ili kuendana na mabadiliko yanayotokea ulimwenguni kote na ndani ya jamii.

Prof. Elifas Bisanda, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) ametoa kauli hiyo wakati wa mafunzo ya uandaaji na ukuzaji mitaala kwa wakuu wa vitivo, wakurugenzi, udhibiti ubora, Taasisi ya Elimu Endelezi na wakuu wa idara zote za kitaaluma kutoka vitivo vyote vya OUT.

Mafunzo hayo yalifanyika katika Shule Kuu ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere iliyoko Kwa Mfipa, wilayani Kibaha, mkoani Pwani kuanzia Agosti 24 hadi 26 mwaka huu.

"Nchi yetu ipo katika kufanya mabadiliko ya mitaala katika katika ngazi za elimu ya msingi na sekondari ambayo kwa sasa imefika mahali pazuri.

"Na sisi watu wa vyuo vikuu, OUT ikiwamo, tupo katika kuimarisha mitaala yetu ili iendane na mabadiliko hayo pamoja na hali ya soko na mahitaji ya ajira katika jamii.

"Ndiyo maana leo tupo hapa Kibaha kwa ajili ya kuwanoa wakuu wote wa idara ili nao wakawanoe wahadhiri katika idara zao. Ni lazima tuhakikishe tunakuja na mitaala ambayo itazalisha wataalamu wenye uwezo wa kujiajiri na kubuni miradi ambayo itaajiri wenzao," alisema Prof. Bisanda.

Akimshukuru Makamu Mkuu wa Chuo kwa hotuba nzuri ya ufunguzi wa mafunzo, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu, Prof. Deus Ngaruko, alisema kunahitajika mitaala yenye kulenga kutoa ujuzi ili wahitimu watoe maarifa, nyenzo na kubadili mtazamo wa kusubiri kuajiriwa, bali kujiajiri.

"Ujuzi ndiyo jambo la msingi kwa sasa. Tunatakiwa tuhakikishe wahitimu wetu wanaweza kufanya nini kipya na siyo kujua nini peke yake. Kujua tu halafu kushindwa kufanya kitu kipya haikubaliki katika ulimwengu huu ambapo sasa elimu na maarifa imekuwa ni jambo mtambuka.

"Tunakushukuru sana Makamu Mkuu wa Chuo kwa kuwezesha mafunzo haya muhimu katika kipindi hiki tupo kwenye mapitio ya mitaala," alisema Prof. Ngaruko.

Mbobezi wa Masuala ya Mitaala, Prof. Paul Mushi, alishiriki katika kutoa mafunzo kwa wakuu hao wa idara katika eneo la usanifu wa mitaala.

Miongoni mwa aliyofundisha ni kuwataka waandaji hao wa mitaala kuhakikisha wanafanya utafiti wa kutosha ili kuja na mitaala ambayo inakidhi mahitaji ya jamii ya sasa na baadae.

Pia alisisitiza kufahamu malengo na mipango ya serikali, sera za serikali, misingi ya taifa, utamaduni wa jamii ya Kitanzania, miiko na maadili katika nchi na ulimwengu kwa jumla.

## Mbaroni akidaiwa kuua mkewe

**Na Timothy Itembe,**

TARIME

JESHI la Polisi Mkoa wa Kipolisi Tarime/Rorya, linamshikilia Silasi Kokolo (50), mkazi wa Kemonge, kwa tuhuma za mauaji ya mke wake Furaha Silasi (47), aliyemshambulia kwa mapanga mwilini na kumsababishia kifo kutokana na madai ya wivu wa mapenzi.

Kamanda Mkoa wa Kipolisi Tarime /Rorya, Marco Njera, aliiambia Nipashe jana kuwa tukio hilo lilitokea Agosti 29, mwaka huu majira ya saa mbili asubuhi, wakati wakiwa njiani kuelekea nyumbani kwao.

"Tunamshikilia Silasi Kokolo, mkazi wa Kemonge kwa ajili ya upelelezi zaidi akikabiliwa na tuhuma za mauaji ya mke wake kwa kumkata mapanga sehemu mbalimbali za mwili chanzo cha tukio hilo ni wivu wa mapenzi," alisema Kamanda Njera.

Alisema, upelelezi ukikamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kujibu mashtaka na kuitaka jamii kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi.

"Kuhusu sababu ya ugomvi wao, mtuhumiwa bado anaendelea kuhojiwa kwa kina na jeshi letu na tukishapata ushahidi wa kutosha atafikishwa mahakamani kujibu mashtaka yake," alisisitiza.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Tarime, Yonam Charles, alithibitisha kupokea mwili wa marehemu akieleza kuwa alimpokea akiwa tayari amefariki dunia baada ya kupoteza damu nyingi katika shambulio hilo.

Alisema mwili huo ulikuwa umekatwa mapanga sehemu mbalimbali za mwili na waliupokea Agosti 29, majira ya saa nne asubuhi na umehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia miili kusubiri kukabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya mazishi.



Kamishna Msaidizi wa Polisi Wilaya ya Temeke, Mairi Makori akipokea gari la polisi kutoka kwa Meneja Uhusiano wa kampuni ya Bima ya Sanlam Life Insurance, Abdallah Ikimbia katika kituo cha polisi Kigamboni, Dar es Salaam jana, baada ya kufanyiwa matengenezo makubwa yaliyogharamiwa na kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

# Mkuu wa Upelelezi ashangaa Wakili Kibatala kuwa na nyaraka za siri za polisi

**Na Grace Gurisha**

MKUU wa Upelelezi Mkoa wa Arusha, SSP David Mhanaya, amemtaka Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, katika kesi ya mauaji ya mdogo wa marehemu Erasto Msuya 'Bilionea Msuya', Aneth Msuya, kumweleza amepata wapi nyaraka za siri za ndani ya Jeshi la Polisi kuhusu taarifa za awali za tukio hilo.

Washtakiwa katika kesi hiyo namba 103 ya mwaka 2018 ni mke wa aliyekuwa marehemu Bilionea Msuya, Miriam Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyela, wote wakazi wa Arusha.

Shahidi huyo namba 22, SSP Mhanaya alitaka ufafanuzi huo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati wakiulizwa maswali ya dodoso na Wakili Kibatala baada ya kumaliza kutoa ushahidi wake.

**Kibatala:** Shahidi hebu shika hii karatasi halafu Mheshimiwa Jaji akishamaliza kuandika, mweleze nyaraka hizo ni za nini na kama unazifahamu.

**Shahidi:** Ninafurahi sana umeniletea karatasi hii ya 'first criminal report' ya taarifa za awali za Jeshi la Polisi. Haya niambie umeitoa wapi?

(Shahidi huyo aliendelea kudai kuwa nyaraka hizo hazipo hata katika maelezo ya mashahidi (committal). Anashangaa kwa sababu taarifa hizo ni za ndani).

Hizi ni taarifa za awali za tukio hili la mauaji, ni za ndani kwa ndani za Jeshi la Polisi, saa nieleze mmezipata wapi? Hebu nieleze.

**Kibatala:** Achana na hayo mambo yote. Mimi nimekuuliza unafahamu hizo nyaraka au hufahamu, huko unapotaka kwenda tutafika tu.

**Shahidi:** Mimi ninataka kujua mmeipata wapi?

**Kibatala:** Unafahamu au haufahamu, kwa sababu hicho ni kielelezo cha mahakama, nimekiomba mimi hapa.

**Shahidi:** Sifahamu

**Kibatala:** Umeona sasa faida ya kuongea mambo mengi sana. Unajua kama nyaraka hizi zilitolewa na askari mwenzako ambaye alisukumwa kuzitoa?

**Shahidi:** Sifahamu

**Kibatala:** Soma hizo nyaraka, sasa uieleze mahakama mshitakiwa anaitwa nani?

**Shahidi:** Ndiyo maana nikakuuliza 'document' hii umeitoa wapi?

**Kibatala:** Nimeshakujibu kuwa askari mwenzio ndiye alitoa hapa mahakamani.

**Shahidi:** Hii 'document' mimi siitambui.

**Kibatala:** 'Accused' anaitwa nani?

**Shahidi:** Any way Getruda Mfuru.

**Kibatala:** Haya soma na other accused person.

**Shahidi:** Siwezi kusoma kwa sababu handwriting (mwandiko) ninaona kama yameingizwa.

**Kibatala:** Jina la kwanza ni nani nitajie majina.

**Shahidi:** Sabri Kombo Haji, Wilbert Metthew Kimaro na Amiri.

**Kibatala:** Unafahamu kama Kimaro alikuwa ni mume wa marehemu Aneth na alikuwa na ugomvi wa mtoto wao, Allen?

**Shahidi:** Siwezi kulizungumzia hilo, sifahamu.

**Kibatala:** Yeah! Ni bora useme hufahamu kuliko kusema hivyo, kwa sababu tutaona kama una jeuri.

**Shahidi:** Wewe usiniambie mimi kuwa nina kiburi, kuwa na heshima wewe.

**Kibatala:** Katika ushahidi wako ulieleza kuwa uliende eneo la tukio na mlikuta milango imevunjwa. Je, mliwauliza majirani kama walisikia milango inavunjwa?

**Shahidi:** Tuliwauliza, lakini walisema hawakusikia chochote.

**Kibatala:** Ulikuwa unafahamu kama Getruda alikuwa anamsumbua bosi wake akidai aongezwe mshahara na pia alikuwa na wanaume wengi?

**Shahidi:** Sifahamu.

**Kibatala:** Ulikuwa unajua kama Aneth alikuwa ana mpango wa kumrudisha kwao?

**Shahidi:** Sifahamu kwa sababu sikuongea na marehemu.

**Kibatala:** Hebu ieleze mahakama binti huyu alikuwa ana miaka mingapi ili tujue kama alikuwa amekomaa au la.

**Shahidi:** Sikumbuki ni muda mrefu ila kitu kitachonijulisha umri ni kwamba alikuwa ni mama wa watoto watatu.

**Kibatala:** Mtu mwenye watoto watatu anashindwa kutoa taarifa polisi, anakwenda kumwambia 'boyfriend' wake?

**Shahidi:** Mheshimiwa Jaji, kila mtu ana ufahamu wake wa kupambanua mambo.

**Kibatala:** Ulijiridhisha vipi kama Getruda alipewa na 'boyfriend' wake Sh. 50,000 kama nauli?

**Shahidi:** Ni kwa sababu alisafiri kwenda kwao Moshi Masama na hata tulipomtafuta tulimkuta huko.

**Kibatala:** Nikurudishe nyuma kidogo, katika ushahidi wako ulisema kwamba uliagizwa na DCI nani kwenda kuongeza nguvu?

**Shahidi:** Kamishna Diwani Athuman

**Kibatala:** Ni Diwani Athuman Msuya?

**Shahidi:** Mimi sifahamu. Ninajua ni Diwani Athuman.

**Kibatala:** Haya niambie anatokea mkoa gani?

**Shahidi:** Sifahamu

**Kibatala:** Na huyu ASP Mchovu naye anatokea mkoa gani au na huyu hujui pia?

**Shahidi:** Sijui

**Kibatala:** Hebu shika karatasi hii ya upekuzi nyumbani kwa mtuhumiwa namba mbili, halafu uisomee mahakama hapo mwishoni jina lililoandika.

**Shahidi:** Nimeandika Revocatus Mollel, kwa sababu kwenye kichwa changu kulibaki jina hilo wakati ninarekodi vielelezo, cheti cha mgambo cha mtuhumiwa kilikuwa na jina hilo, lakini awali niliandika Revocatus Muyela.

**Kibatala:** Nimesikia hapa ukizungumzia kuhusu Arusha. Hebu mwoneshe jaji na wazee wa baraza kwenye hiyo karatasi kama kuna sehemu inaonesha upekuzi ulifanyika Arusha.

**Shahidi:** Hapa kuna Olasiti, ipo Arusha. Usinilizamishe, ukiwa unaniuliza niulize kwa heshima.

Jaji: Hebu jibu swali, Arusha ipo au haipo?

**Shahidi:** Neno Arusha halipo.

**Kibatala:** Nikurudishe nyuma tena, wakati mnafanya upekuzi katika nyumba ya Muyela, mlisema mlikuta bastola. Je! mliwahi kufanya utambuzi wa bastola hiyo kwa Getruda?

**Shahidi:** Sikuona umuhimu

**Kibatala:** Hiyo briefcase mliyoichukua kwa mtuhumiwa namba mbili, mliomwonesha Getruda ili aitambue?

**Shahidi:** Nilimwonesha lakini hakuitambua

**Kibatala:** Hizo simu tatu za mtuhumiwa mlizichukua mlizifanyia uchunguzi?

**Shahidi:** Tulizifanyia uchunguzi, lakini hatukuzikuta na kitu kwa sababu simu walizotumia kwenye 'mission' yao ni zingine.

**Kibatala:** Ooh

**Shahidi:** Wewe huwezi kuwa polisi kama mimi, lakini mimi ninaweza kuwa advocate kama wewe.

**Kibatala:** We thubutu!

**Kibatala:** Jeshi la Polisi lina mamlaka ya kupata taarifa za mawasiliano ya simu. Je, mliwahi kuiomba kampuni yoyote ya simu mawasiliano kati ya Revocatus na Miriam?

**Shahidi:** Tulifanya sana jitihada kuhusu simu za watuhumiwa, lakini zilionekana hazijatumika katika tukio la mauaji.

**Kibatala:** Katika ushahidi wako, ulisema Getruda alinunuliwa simu na watuhumiwa. Je, hadi leo ulishawahi kuzijua namba hizo?

**Shahidi:** Sizifahamu

Miriam ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi hiyo ya mauaji hayo ya wifi yake, Aneth, aliyeuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake Kibada, Kigamboni, Dar es Salaam, amekiri kuhusika na mauaji hayo katika maelezo yake ya onyo.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mkopo wa kuunganisha maji utanufaisha wengi

**AGIZO** la serikali la kuitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kuwaunganishia wananchi maji kwa mkopo litawakomboa wengi ambao hawakuwa na uwezo wa kulipia gharama kwa mkupuo.

Wananchi wanaotarajiwa kunufaika na mkopo huo ni wale wanaoishi kwenye maeneo ya Mradi wa maji wa Chalinze awamu ya tatu ambao kwa sasa umekamilika.

Wananchi hao wa kijiji cha Kihangaiko, Kata ya Msata, Halmashauri ya Chalinze Wilaya ya Bagamoyo walipata taarifa hizo njema kwenye mkutano wa hadhara uliofanywa na Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, aliyefanya ziara ya kukagua upanuzi wa mtambo wa kuzalisha maji wa Wami.

Mradi huo umetekelezwa kwa juhudi za Rais Dk. Samia Suluhu za kuhakikisha adhma ya kumtua mama ndoo kichwani inafanyika kwa vitendo.

Pongezi pia ziwafikie watendaji wa DAWASA kwa utekelezaji wa wa mradi huo ambao utawakomboa wananchi wengi na tatizo la upatikanaji wa majisafi na salama.

Agizo la kuwaunganisha wanufaika wa mradi huo kwa mkopo linatakiwa kuzingatia masharti nafuu na vigezo rafiki ili kila mwananchi apate huduma ya majisafi karibu na makazi yake.

Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Halima Okashi aliipongeza Wizara ya Maji kwa kusimamia vyema utekelezaji wa miradi ya maji katika Wilaya ya Bagamoyo hususani mradi wa maji wa Chalinze awamu ya tatu.

Mradi huo ni muhimu kwa kuwa unaenda kuondoa kero ya upatikanaji wa maji iliyokuwapo kwa mda mrefu.

Rais Samia ameonyesha kuwajali wananchi wake hasa kinamama ambao wamekuwa wakipata tabu kubwa ya kutafuta maji umbali mrefu na wakati mwingine baadhi yao kuathiri ndoa zao.

Upatikanaji maji katika Wilaya ya Bagamoyo sasa unaelezwa kuwa ni wa uhakika na DAWASA kwa kuendelea kuipa ushirikiano ofisi ya Mkuu wa wilaya kwa kuzunguka kata zote 26 kusikiliza na kutatua changamoto za wananchi wa wilaya hiyo.

DAWASA inasema mradi wa maji wa Chalinze ni moja ya miradi ya mfano ya vijijini kutokana na usanifu mzuri uliofanyika na utaenda kunufaisha takribani vijiji 59 vya Pwani, Morogoro vijijini na Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga.


Mradi wa maji wa Chalinze awamu ya tatu umehusisha upanuzi wa mtambo wa kuzalisha maji Wami, ulazaji wa bomba za inchi 12 na 16 kwa umbali wa kilomita 24, ujenzi wa matangi ya kuhifadhi maji ya chini na juu takribani 19 na ujenzi wa vizimba vya kuchotea maji takribani 351 na umegharimu zaidi ya Sh. bilioni 44 ambao utanufaisha wakazi zaidi ya 200,000

Diwani wa Kata ya Msata, Celestin Mcholo, aliishukuru kwa serikali kupitia DAWASA kuwaletea mradi mkubwa wa maji ambao umeleta mabadiliko makubwa pia amemshukuru Naibu Waziri kwa kupokea kilio chao cha kufanyiwa maunganisho ya maji kwa mkopo.

Ni matarajio kuwa wananchi wa Kata ya Msata wataitunza miundombinu na vyanzo vya maji ili kuendelea kupata huduma ya majisafi bila changamoto yoyote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tuwanusuru wa mabondeni

Na Tuntu Abed

**HIVI** karibuni Mamlaka ya Hali ya Hewa imetahadharisha kuwapo kwa mvua kubwa za El Nino, angalizo hilo linapotolewa linakuwa mwiba kwa wakazi wa maeneo yenye mafuriko mijini na vijijini ambao wanapitia adha nyingi ikiwamo kupoteza maisha.

Mathalani, kipindi cha mafuriko jijini Dar es Salaam wakazi wa Boko Basihaya hupatwa na adha kubwa kwa vile kwanza wengi hawaamini mpaka kushuhudia mafuriko yakiwazidi , maji kuwazingira ndani na nje hivyo kushindwa kuokoa mali zao na jitihada zikiwa kunusuru maisha yao.

Wengi hukimbia makazi yao na kutafuta hifadhi sehemu mbalimbali kama kwa marafiki, jamaa na ndugu zao lakini nyuma au nyumbani mali zao zikiharibika kuanzia samani, vyakula, bidhaa madukani, pesa, mazao kama mboga na matunda wanayozalisha na vyote hupotea kwa siku chache na wanaporudi kwenye maeneo yao hawana chochote na kulazimika kuanza upya utafutaji.

Vitu muhimu kama vyeti vya masomo , ndoa, hati mbalimbali zinazohusu mauzo na manunuzi ni miongoni mwa vinavyoharibiwa na mafuriko hata wanyama wakiwamo kuku na mifugo mingine hupotea pia. Hii ni adha na uchungu kwa wakazi wa maeneo hatarishi kwa mafuriko.

Mafuriko ni chanzo cha vifo na kukwamisha shughuli za kijamii kwa familia ambazo watoto wake ni wanafunzi wanapohamia maeneo mengine inamaanisha kuwa watakuwa mbali na shule, hivyo kulazimika kukatisha masomo kwa muda ili kuweka mambo sawa.

Aidha, wakati huo wa mafuriko ikumbukwe adha zinazoambatana na kukimbia makazi na kutafuta hifadhi sehemu nyingine watoto hao walio wengi hawawezi kwenda shule kwa sababu ya umbali, kukosa mavazi, vitabu na daftari vyote kuharibiwa na maji.

Halikadhalika baada ya mafuriko watoto hawa wanaporudi shuleni huwa nyuma kimasomo kwani kipindi chote cha mafuriko walikuwa hawapati muda wa kujisomea hivyo wakati mwingine kuchangia kufeli mitihani yao.

Athari za mafuriko ni nyingi na hazisemeki ila kukinga ni bora kuliko kuponya. Hivyo wakati angalizo la mvua kubwa na El Nino likitolewa wananchi waelekezwe kutengeneza mitaro mikubwa ili kupitisha maji yanayowasumbua wakazi wa sehemu zilizo karibu na mikondo ya maji, mabondeni na mtoni.

Pamoja na hayo ni vyema pia kuweka mkazo wa kushirikiana wadau kujenga mitaro itakayopokea maji ya kuzuia maili yasielekee kwenye makazi ya watu na kuhimiza kuta na majengo yanayozuia maji kuondolewa kwa sababu athari za mafuriko ni kubwa kwa maisha ya watu kuliko ukuta au majengo ya wafanyabiashara.

Ni taabu kwa wengi kurejea na kuanza maisha upya baada ya mafuriko kwa vile wakazi hawa wanaporejea makwao mazingira huwa machafu kupindukia yakiwa na vinyesi taka za vyooni, kemikali za sumu, taka za viwandani ambazo zimejaa vyumbani na viwanjani kutokana na maji kutuama.

Watanzania hawa hata wanapofanya usafi bado hawawezi kuumaliza kwani uchafu ni mwingi na wanalazimika kukaa kwenye maeneo machafu na hatarishi kwa maisha.

Wakazi hawa hasa upande wa kina mama hulazimika kuoshea vyombo kwenye viwanja vichafu, kupika na kuandaa mlo kwenye maeneo hatarishi na kuona watoto wakicheza sehemu zilizokuwa zimelundikana vinyesi na taka hatarishi.

Hali hii ni hatari kwa watoto kupata magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu, homa za matumbo na wakati mwingine kichocho na kuwalazimu wazazi na walezi kutumia pesa nyingi kuwatibu.

Kukabili mafuriko ni muhimu kwani kwa upande mwingine shughuli za kutafuta pesa wakati huo husimama na kuwapa wakazi hawa wakati mgumu wasijue wapi pa kupata mahitaji ya kujikimu na familia zao.

Inawezekana kutokea familia kutelekezwa kutokana na kukosekana fedha na watoto wakawa waathirika wakubwa.

Ni vyema sasa serikali na wadau wakaelekeza na kuchukua tahadhari pamoja na wakazi wa maeneo hatarishi kwa mafuriko ili kuepusha hatari zinazoweza kuja na El Nino.

HABARI KITAIFA

# Wafugaji waomba kufikiwa na BBT

**Na Maulid Mmbaga**

VIJANA wanaojihusisha na ufugaji nchini wameiomba serikali kuwafikiria kwa kuwaanzishia programu kama ya Jenga Kesho Bora (BBT) kwenye kilimo ili iwasaidie kwenye shughuli za ufugaji.

Serikali ilianzisha programu ya BBT kwa lengo la kuwakwamua vijana wanaojihusisha na shughuli za kilimo, ambapo jana Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alitangaza wahitimu 763 waliopatiwa mafunzo kupitia programu hiyo watapewa mashamba mkoani Dodoma na kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa mwezi mmoja.

Akizungumza na Nipashe, Omari Mhina, ambaye ni mwakilishi wa vijana wanaoshiriki mradi wa Tanga yetu unaojihusisha na ufugaji wa kuku, alisema wamepatiwa mafunzo ya ufugaji, lakini wanashindwa kuendelea kwasababu ya changamoto ya ukosefu wa mtaji wa kununua maeneo pamoja na baadhi ya vifaa kwaajili ya kuendeshea shughuli za ufugaji.

"Kupitia mradi huu umetufungua akili na tunafikiria kufanya vitu vingi na vikubwa, lakini kwa bahati mbaya mazingira yanatukwamisha, changamoto ni nyingi, sisi ni vijana ambao bado hatujafanikiwa kujiendeleza katika suala la ardhi na mitaji," alisema na kuongeza;

"Tunatamani twende tukafuge, lakini uwekezaji wa kufuga unahitaji ardhi na sisi asilimia kubwa bado hatujafikia hatua ya kumiliki eneo, kwetu hii ni changamoto ambayo kila kukicha tunakaa tunawaza, tunafanyaje, tunapata wapi eneo," alisema Mhina.

Pia, suala la kufuga ni uwekezaji mkubwa ambao unaghariмu fedha nyingi, na wamekuwa wakishiriki mafunzo ya vitendo katika kampuni ya Ufugaji na Maendeleo ya Vijana na Wanawake Vijijini (AKM) kwaajili ya kujiimarisha zaidi kuielewa na kujipatia kipato ambacho wanakitumia kununua baadhi ya vitu vitakavyowasaidia katika ufugaji.

Alisema mikopo inayotolewa kwa vijana ikiwamo ya halmashauri inaishia katika kununua baadhi ya vitu kama vifaranga, dawa, vyakula na vifaa, lakini haitoshelezi katika kununua ardhi na kutekeleza ujenzi wa mabanda.

Hata hivyo, alibainisha kuwa wanashiriki pia miradi mbalimbali ambayo lengo lake ni kumsaidia kijana atoke aliko na aweze kufikia kiwango cha kujitegemea kupitia fursa zilizopo kwa upande wa ufugaji.

Zaituni Chausa, mshiriki wa mradi wa Tanga yetu, alisema baada ya kupata mafunzo wamekuwa wakipita maeneo mbalimbali nyumba kwa nyumba kwaajili ya kuwaelimisha wanajamii juu ya suala la ufugaji wenye tija na manufaa yake ili waweze kujikwamua kiuchumi.

"Tunataka tukimaliza huu mradi tusiishie hapa, lakini changamoto kubwa ni ardhi kama mwenzetu alivyosema, tunataka tuonyeshe serikali kwamba vijana tunaweza tumepatiwa elimu na mafunzo kwa vitendo, tunatamani kuleta mapinduzi katika ufugaji japo kuna vitu vinatukwamisha ambavyo tuna imani vikipatiwa ufumbuzi tutasonga mbele," alisema Zaituni.

Mkurugenzi wa kampuni ya AKM, Elizabeth Swai, alisema wanawapatia mafunzo vijana 50, yanayohusu ufugaji, mikakati ya biashara na kujitambua, pamoja na kuwawezesha fedha watakayokwenda kuitumia kama kianzio kwenye shughuli za ufugaji.

Alisema vijana hao watakuwa na fedha ya mtaji, lakini watakosa ya kujenga mabanda, na AKM imetafuta njia ya kuwaendeleza kwa kuungana na shirika linalojihusisha na Ufadhili wa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati (EFTA) ambalo limekuja na programu ya kuwakopesha wafugaji kuku.

"Mkopo huo ni wa masharti nafuu kwasababu auhitaji kuweka mali au ardhi, hivyo utaendeleza vijana katika 'level' tofauti na mpaka sasa kuna ambao wameshakodisha mabanda kwaajili ya kupokea vifaranga mwezi ujao kwaajili ya kuendelea na ufugaji.

"Tumewatambulisha EFTA na wamekubali kuwabeba lakini tatizo watapata shida kwasababu ili upate mkopo labda wa Sh. milioni mbili lazima asilimia 25 uwe nayo ili EFTA wakupe 75, sasa hiyo kwa vijana ni tatizo," alisema Elizabeth.

Vile vile, alitoa wito kwa serikali pamoja na wadau wengine kutowaacha vijana hao kwasababu wanahitaji kuendelezwa hasa katika suala la ardhi kama walivyofanyiwa wanaojihusisha na kilimo ambao wamepatiwa hekari 10.

## 260 wapelekwa Israel kujifunza kilimo, teknolojia

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imesema jumla ya vijana 260 wanapelekwa nchini Israel kupata mafunzo yatakayowapatia ujuzi na uzoefu katika masuala ya kilimo kwa kutumia teknolojia za kisasa.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Jamal Katundu, wakati wa halfa ya kuwaaga vijana hao ambao baadhi wameanza kuondoka kwa makundi tofauti tofauti.

Alisema mafunzo hayo ya uzoefu na ujuzi wa kilimo cha kisasa yanatoa nafasi kwa vijana kufahamu mbinu za kilimo kinachotumia teknolojia za kisasa ili waje kutumia mbinu hizo wanaporejea nyumbani lengo kuongeza tija na ubora wa mazao na mifugo kwa ujumla.

"Kitendo hiki kinasaidia kuimarisha uzalishaji na ufanisi katika sekta mbalimbali na hivyo kuboresha maslahi ya wananchi na kuongeza pato la taifa," alisema Katundu.

Alisema utafiti wa nguvukazi wa mwaka 2020/21 ulionyesha asilimia 65.6 nguvu kazi ya taifa inafanya shughuli za kiuchumi katika sekta ya kilimo.

Katundu alisema inaonyesha wazi kuna umuhimu wa kuongeza juhudi na kuhakikisha sekta ya kilimo inakuwa na watu wenye ujuzi wa kutosha haswa katika matumizi ya teknolojia ya kisasa, ili kuongeza tija na ubora wa mazao katika sekta hiyo.

Aidha, alisema ofisi yake inatekeleza programu ya taifa ya kukuza ujuzi ni mahususi katika kuhakikisha nguvukazi ya taifa inapata ujuzi stahiki, ili waweze kujiajiri na kuajiriwa.


The Guardian Limited

JOB VACANCY

The Guardian Limited, **Publishers of leading Tanzanian newspapers, The Guardian, Nipashe and Nipashe Jumapili, is looking for motivated and experienced people to fill the position of:**

SENIOR MARKETING EXECUTIVE – DAR ES SALAAM

**Job Purpose:**

Developing and executing strategies to promote brands, products and services, maximizing profits for the company.

**Main Responsibilities:**

- Formulate an appropriate commercial strategy that responds to the overall development of the company's marketing operations, newspaper sales, advertisements and other printed products.
- Become knowledgeable expert of The Guardian Limited products and be experienced in identifying target markets and developing strategies to communicate with them.
- Identify, plan, prepare and produce proposals for the targeted audiences.
- Study competitors' products and services on a daily basis, with a view to designing counter strategies.
- Advise clients on their advertising and promotion campaigns.
- Organize all company events related to CSR, promotion, product launching, staff parties, etc.
- Monitor and analyze product performances, trends and provide accurate reports on programe and market information.
- Explore ways of improving existing products and services and increasing profitability.
- Advise the Management with feasibility studies on ways to get sponsorship for various events, highlighting benefits to the Company.
- Engage in negotiating and closing deals where and if appropriate.
- Prepare periodic performance reports for the Management and provide appropriate inputs towards improvement and the taking of remedial measures.
- Design and implement human resources training and development programme

**Minimum Qualifications and Experience:**

- University Degree in Business Administration/Sales & Marketing or equivalent.
- At least 5 years' relevant working experience.
- Excellent communication skills, computer knowledge and familiarity with a wide range of newspaper brands.

**MODE OF APPLICATION:**

Apply online via email address: **vacancy@guardian.co.tz** by **8th September, 2023.**

**NB:** Only shortlisted candidates will be contacted.

*Please note that The Guardian Limited is an equal opportunity employer.*

# Ubalozi waanza kumsaidia Mtanzania aliyekwama India

**Na Emmaloveness Gaston**, TUDARCo

BALOZI wa Tanzania nchini India, Anisa Mbega, amesema ofisi yake inafanya jitihada za kumsaidia Sayuni Eliakim kwa kumpatia hati ya kusafiria ya dharura (ETD).

Awali, Eliakim ambaye anaishi India inasemekana alishidwa kusaidiwa ubalozini hapo kupata hati ya kusafiria ili arudi Tanzania na kutakiwa kufanya maombi kwa njia ya mtandao.

Ufafanuzi huo ulitolewa jana zikiwa ni siku mbili tangu taarifa za Eliakim ambaye alinyanyang'anywa hati ya kusafiria na mwenyeji wake kukosa huduma ubalozini hapo.

Balozi Mbega alifafanua kuwa Sayuni alizidisha muda wa kibali chake cha ukaazi nchini humo, hivyo kuna ugumu katika mchakato wa kumrudisha Tanzania.

"Ubalozi wa Tanzania nchini India tunafanya jitihada ili kumpatia hati ya kusafiria ya dharura (ETD) kutokana na sheria, kanuni na taratibu za uhamiaji za India. Raia wa kigeni ambaye amepitisha muda wake wa ukaazi, haruhusiwi kutoka nchini India, isipokuwa kwa utaratibu maalum uliowekwa," alibainisha Balozi Mbega.

Alisema Eliakim aliingia India mwaka 2018 na kukaa kwa muda mrefu hadi kujikuta muda wake wa ukaazi umepita. Ili kurudi Tanzania, alitakiwa kuomba ruhusa ya kutoka nje ya nchi (Exit Permit0 inayofanyika katika mji ambao mhusika anaishi).

Vile vile, Balozi Mbega alisema msichana huyo anaishi mji wa Bangalore na pia alielekezwa kuhusu utaratibu huo na maombi yake hadi hivi sasa yanaendelea kufanyiwa kazi na yakikamilika atapatiwa hati hiyo.

Aidha, ubalozi umetoa rai kwa Watanzania kujiepusha na kuchukua tahadhari na watu wasio waaminifu wanaowalaghai kuhusu kuwepo kwa nafasi za ajira zisizo na ujuzi kwa raia wa Tanzania nchini India.



Rais Samia Suluhu Hassan akikata utepe kufungua rasmi jengo la ukumbi wa kufanyia mitihani pamoja na chumba cha kompyuta katika skuli ya sekondari ya Muyuni, mkoa wa Kusini Unguja, Zanzibar juzi, lililojengwa kwa ufadhili wa benki ya Azania, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za tamasha la Kizimkazi. Wa nne kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa benki hiyo, Esther Mang'enya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TCU yatoa utaratibu waombaji shahada ya kwanza

**Na Romana Mallya**

TUME ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), imewataka waombaji Shahada ya Kwanza mwaka 2023/24 kuendelea kujithibitisha huku kikiwatoa hofu waliopo katika mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kuwa watapata fursa hiyo.

Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, aliyasema hayo jana akisisitiza hakuna atakayelazimishwa kujithibitisha katika chuo asichohitaji.

Prof. Kihampa alisema kama kuna mwombaji atakwama katika hatua zozote wakati wa udahili au uthibitisho, awasiliane na TCU kwa kupiga simu au kuandika barua pepe.

Aliwakumbusha waombaji kuwa uthibitisho ufanyike kupitia akaunti za kielektroniki ambazo (mwombaji) alifungua kwa vyuo husika.

Alisema suala hilo halifanyiki kwa simu wala kwa fomu maalum, bali kwa mwombaji kuingia kwenye akaunti ambayo waliomba kudahiliwa.

"Wapo ambao wamejithibitisha kwenye chuo X, lakini baadaye wamebadili mawazo na kutaka chuo Y. Basi watumie ujumbe wa kwenye simu afute uthibitisho wake na aende kujithibitisha katika chuo anachokitaka," alisema.

Alisema wanaotaka kubadili maombi yao ya udahili, wanapaswa kuingia katika akaunti zao za vyuo walivyodahiliwa na kufuta udahili wao ili kutuma upya maombi.

"Mpaka sasa jumla ya waombaji 23,387 waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja kati ya 43,213 wameshajithibitisha katika chuo kimoja wapo.

"Kwenye kipindi hiki kuna watu ambao siyo waaminifu wanaoweza kujitambulisha kama maofisa udahili wa chuo fulani tunahimiza vyuo vyote vijitangaze kuelezea mawasiliano yao sahihi," alisisitiza.

Alisema baada ya dirisha la pili kufungwa litafunguliwa la awamu ya tatu itakayokamilika Septemba 29.

# Wanaotaka mkopo elimu ya juu waondolewa hofu

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa hakuna ugumu kwa wanafunzi waliosoma shule binafsi kupata mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu iwapo muomboji atafuata maelekezo yote na kukidhi vigezo husika.

Aidha, mapitio ya utoaji mikopo hiyo inaendelea na inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu na kuwezesha Bodi kuwa na sheria na miongozo inayoendana na wakati wa sasa.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti maalum (Chadema), Sophia Mwakagenda.

Mwakagenda alihoji, kumekuwa na ugumu wa upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi waliosoma shule binafsi wanapojiunga na elimu ya juu. Akijibu swali hilo, Kipanga alisema mikopo inayotolewa na serikali kupitia bodi hiyo inawalenga vijana wenye sifa za kitaaluma za kujiunga na taasisi za elimu ya juu, lakini hawana uwezo wa kumudu gharama za elimu.

Aidha, alisema upangaji na utoaji mikopo unaongozwa na Sheria ya Bodi ya Mikopo (SURA 178) kwa kuzingatia sifa za msingi ambazo ni awe Mtanzania, amepata udahili wa masomo ya shahada au stashahada katika taasisi inayotambuliwa na serikali.

Pia, alisema asiwe na vyanzo vingine vinavyogharamia masomo yake na kwa wanaoendelea na masomo ya mwaka wa pili, watatu na kuendelea, wawe wamefaulu kuendelea na masomo yao katika mwaka unaofuata.

"Kila mwaka Bodi huandaa mwongozo unaopaswa kuzingatiwa na waombaji na kuweka masharti ya utoaji mikopo kwa mwaka husika. Pamoja na vigezo vilivyotajwa, mwongozo huelekeza taratibu za kufuata wakati wa kuomba mkopo pasipo kuangalia mwanafunzi kasoma shule ya binafsi au ya umma," alisema.

"Mheshimiwa Spika, iwapo muomboji atafuata maelekezo yote kama yalivyo katika mwongozo wa mwaka husika na akawa ana vigezo vyote, hatutegemei pawepo na ugumu wowote katika kupata mkopo hata kama alisoma shule binafsi."

Kadhalika, alisema serikali imeendelea kuongeza fedha za mikopo ya wanafunzi hao kutoka Sh. bilioni 464 mwaka 2021/22 hadi Sh. bilioni 738 kwa mwaka 2023/24 ili wanafunzi wapate mikopo.



## Serikali yajipanga kutoa intaneti ya bure kila sehemu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI ipo mbioni kuimarisha huduma za mawasiliano nchini, kwa kuweka mtandao wa intaneti bure (WiFI) kwenye mikusanyiko yote, vyombo vya usafiri na kwenye shule ili kila mwananchi apate huduma hiyo bila usumbufu wowote.

Akizungumza jana jijini Arusha, Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Methew Kundo, alisema uwekaji huo wa intaneti za bure, zitasaidia wananchi kupata huduma za mawasiliano popote wanapokuwa na kuendelea na shughuli zao za kijamii, bila mkwamo wa ukosefu wa huduma hiyo.

Alikuwa akizungumza na wadau mbalimbali, wakati akifungua kikao cha 41 cha Baraza la Utawala la Umoja wa Posta Afrika (PAPU).

Kundo alisema: "Hapa tunataka hakikisha katika umoja huu, tunaboresha mifumo ya utendaji kazi na kuwa ya kidijitali na sisi kama Tanzania, tukiwa wanachama wa umoja huu Afrika na duniani, tumeanza fanya vizuri kwa kuanza na utekelezaji wa makubaliano, tuliyojiwekea kwenye umoja wetu wa Afrika na duniani, kwa kuweka sawa sera yetu ya posta ya mwaka 2003 kwa kuboresha miundombinu ya mawasilino."

Alisema mojawapo ya maboresho hayo ni ujenzi wa minara, mkongo wa taifa na uwekaji wa anuani za makazi, ili kuhakikisha shughuli zote za posta zinafanyika vizuri na wananchi wanapata huduma za kijamii bila usumbufu.

Alisema Rais Samia Hassan Suluhu Februari 8 mwaka jana alihakikisha Tanzania kunakua na anwani za makazi na hilo lilifanyika kwa ufanisi, ambapo kwa sasa kila mmoja anaona faida yake katika upatikanaji wahuduma za kijamii na hata posta inakua rahisi.

"Zamani mtu ukikosea anwani ya mtu kifurushi au barua inapotea inaenda mkoa mwingine, lakini sasa haiwezi kutokea kitu kama hiko, hivyo hii ni hatua kubwa tumepiga, kuelekea tunakotaka katika uimarishaji wa mawasiliano nchini," alisema.

"Tunavyoelekea kutoa huduma zote kidijitali ni lazima kuhakikisha uwezo wetu kimtandao unakua imara ili ifike mahali, kila mmoja asione umuhimu wa kutembea na fedha tasilimu, bali kadi tu na kupata kila aina ya huduma mtu anayohitaji kupata," alisema.

Alisema lengo lao kubwa kupitia PAPU nchi zote za Afrika, zitembee pamoja na isiwepo nchi yoyote itakayobaki nyuma kwenye utoaji wa huduma za mawasiliano

Mwenyekiti wa Baraza la Utawala la PAPU, Richard Ranarison, alisema umoja huo unakusudia kutoa huduma bora na kwa wakati kwa kila nchi na ili kufikia lengo hilo, kila wanapokutana kwenye vikao vyao vya kila mwaka wanaangalia wapi walipo na wanapoelekea na penye dosari wanazirekebisha.

# Bil.9/- hutumika kutoa mafunzo ya uanagenzi kila mwaka

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

KILA mwaka mafunzo ya uanagenzi yanayotolewa kupitia programu ya kukuza ujuzi iliyopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, inayolenga kufungua fursa nyingi za ajira kwa vijana, hutafuna Sh. bilioni tisa.

Mkurugenzi Msaidizi, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia Ukuzaji wa Ujuzi, Robert Masingiri, aliyasema hayo jana alipokitembelea Chuo cha Taifa cha Utalii, Tawi la Arusha.

Mpaka kufikia sasa, vijana zaidi ya 130,000 nchini, wamenufaika na programu hiyo ya miezi sita, hasa kwa wale wanaojishughulisha na ufundi umeme wa majumbani na viwandani, umeme wa jua, useremala, ufundi magari, umeme wa magari, uchomeleaji na uungaji vyuma kwa waliopo kazini.

**Tunafahamu nia ya serikali kuwa ni njema katika kuwasaidia vijana, lakini ningeomba kile kinachotolewa kwa kila kijana, angalau kiongezwe kidogo kama kuna uwezekano.**

Wengine ni wale wa fani za utengenezaji wa vifaa vya aluminium, upishi, uhudumu wa hoteli na vinywaji, ushonaji, uchenjuaji wa madini, ufundi bomba, ufundi uashi, uwekaji wa terazo na marumaru, ufundi viyoyozi na majokofu.

"Programu hii ilianza mwaka 2016, baada ya serikali kukaa pamoja na waajiri, wakakubaliana kuwa ni lazima kuwe na programu ya taifa, ambayo itahusika kukuza ujuzi kwa vijana ili waweze kujiajiri na kuajiriwa.

Kimsingi, programu hii imejikita katika maeneo makuu manne, ambayo ni mafunzo kwa njia ya vitendo, kurasimisha ujuzi mahali pa kazi, mafunzo ya utarajali (internship) na kukuza ujuzi kwa waliopo kazini, kulingana na mabadiliko ya teknolojia."

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, serikali imetenga kiasi hicho cha fedha, ambapo kuanzia Julai imeshatoa Sh. bilioni tano kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

Baada ya ukaguzi huo, Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Utalii, Tawi la Arusha, Dk. Florian Mtei, aliishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kuendelea kutoa fursa hiyo kwa vijana.

Dk. Mtei, alimweleza Mkurugenzi huyo kuwa, moja ya matatizo yaliopo katika utekelezaji wa programu hiyo ni vijana kushindwa kumudu gharama za maisha, ikiwamo chakula na malazi wanapokuwa chuoni.

"Pamoja na ada kulipwa na serikali, lakini wapo vijana wanaoshindwa kuendelea na mafunzo na kuishia njiani kutokana na kushindwa kujikimu kimaisha.

"Tunafahamu nia ya serikali kuwa ni njema katika kuwasaidia vijana, lakini ningeomba kile kinachotolewa kwa kila kijana, angalau kiongezwe kidogo kama kuna uwezekano.

...Hii itawasaidia vijana waweze kumudu gharama za maisha kutokana na wengi kushindwa kumudu gharama za maisha ikiwemo chakula na malazi," alisema.

Mmoja wa wanufaika hao, Jackline Rite, aliomba serikali kuwapatia mkopo kama makundi mengine ya jamii wanapomaliza kozi hizo ili waweze kujiajiri wenyewe.




Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Erasto Mhina (kushoto), akifungua kikao cha baraza la madiwani kilichojadili taarifa ya utekelezaji kazi na uwajibikaji wa halmashauri kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Juni 2023, wilayani humo hivi karibuni. Kulia ni Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## W'biashara mazao ya kilimo wataka leseni moja

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAFANYABIASHARA wanaosafirisha mazao ya kilimo kwenda nje ya nchi, wameitaka serikali kuja na kibali kimoja au leseni, ambayo itaziba mianya ya rushwa mipakani, kuondoa usumbufu na kuepusha hasara wanayoipata ya mazao kuharibika.

Aidha, wameshauri kabla ya serikali kutengeneza leseni au kibali hicho, mchakato wake uwashirikishe kwanza wafanyabiashara mikoa yote.

Wazo la kutaka kuwapo kwa leseni moja ya kusafirisha mazao nje ya nchi, walilitoa jana katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, wakati wakichangia mada kwenye mafunzo maalumu yaliyoandaliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).

Mfanyabiashara, Julieth John, alisema ushirikishwaji wa maamuzi hayo utasaidia kutunza soko la nchi.

Akifungua mafunzo hayo, Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Vedastus Makota, alisema BRELA pamoja na ofisi yake, wamejipanga vizuri kwa ajili ya kupokea kero zao.

"Tuko hapa kwa ajili ya kuwaelimisha wafanyabiashara, kupokea kero zao na kuwasaidia kurasimisha biashara zao ili waweze kufanya kwa urahisi na kwa tija, kunyanyua uchumi wa nchi," alisema Dk. Makota.



# Halmashauri yatakiwa kukamilisha miradi viporo

Na Marco Maduhu, SHINYANGA

HALMASHAURI ya Manisipaa ya Shinyanga imetakiwa kutumia vizuri fedha za miradi ya maendeleo zilizobaki kwa kuhakikisha inakamilisha miradi viporo ambayo haikukamilika katika mwaka wa fedha 2022/23.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Shinyanga, Said Kitinga, alitoa agizo hilo juzi katika baraza maalumu la madiwani, na kuiagiza menejimenti ya halmashauri kwa kushirikiana na madiwani kukamilisha miradi hiyo viporo kwa fedha iliyopo.

**Hadi kufikia June 30 mwaka huu kiasi cha Sh.bilioni 1.3 kilibaki kwa ajili ya utekelezaji wa matumizi ya kawaida na miradi ya Maendeleo.**

Alieleza kuwa katika mwaka wa fedha 2022/23 kuna miradi ambayo bado haijakamilishwa, huku fedha zikiwa zimebaki na kusisitiza ni vyema pesa hizo zitumike kukamilisha miradi viporo.

Aidha, aliitaka halmashauri kulipa madeni ambayo inadaiwa na wazabuni ili waendelee kuwapa uhai wa kutoa huduma tena katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Katika hatua nyingine aliwapongeza watendaji wa halmashauri hiyo kwa kuandaa vizuri taarifa hiyo ya ufungaji wa fedha ambayo ndiyo kipimo cha utendaji kazi wao.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Shinyanga Mjini, Anold Makombe, aliwataka watendaji pamoja na madiwani kuendelea kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuwaletea maendeleo wananchi.

Kaimu Mweka Hazina wa Manispaa ya Shinyanga, Wallace Kiondo, akiwasilisha taarifa hiyo ya kufunga hesabu za mwisho za Halmashauri, alisema katika mwaka wa fedha (2022/2023) halmashauri ilibaki na Sh.bilioni 3.4.

Alisema hadi kufikia June 30 mwaka huu kiasi cha Sh.bilioni 1.3 kilibaki kwa ajili ya utekelezaji wa matumizi ya kawaida na miradi ya Maendeleo.



Mtaalamu wa mnyororo wa thamani kutoka jukwaa la wadau wa kilimo wasio wa kiserikali (ANSAF), Owen Nelson, akitoa mafunzo kwa kongani ya kilimo na wanahabari kuhusu ufuatiliaji, uwajibikaji jamii na uchechemuzi kwa kutumia vyombo vya habari, kwa ufadhili wa The Foundation for Civil Society (FCS) jijini Mwanza jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wazazi, walezi wabanwa malezi bora

Na Mohab Dominick, KAHAMA

WAZAZI na walezi wametakiwa kuhakikisha wanaendelea kutoa malezi bora kwa watoto wao pindi wanapomaliza elimu ya msingi au sekondari ikiwamo kuwasaidia katika taaluma.

Wito huo umetolewa na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo cha Mipango, Fedha na Utawala (TIA) Dk.Hassanal Isaya wakati wa mahafali ya 15 ya Shule ya Sekondari ya Anderlek pamoja na Shule ya Msingi ya Rocken Hill Academy.

Alisema maendeleo ya sayansi na teknolojia sambamba na utandawazi imekuwa sababu ya kushuka kwa maadili ya watoto wakati na baada ya masomo, ikiwa chanzo kikubwa ni wazazi na walezi kutokuweka akilini suala la malezi na kuishia kuangaika maisha.

Hivyo aliwataka wazazi kuwatia moyo walimu ili waweze kufanya kazi yao ya kuwalea watoto vizuri.

Isaya alisema kuwa hakuna kazi kubwa kama ya kuwalea watoto, huku akiwataka walimu kuhakikisha kuwa wanaangalia vipaji walivyonavyo watoto wakati wakiwa shuleni badala ya kuwalazimisha kusomo masomo ambayo hawayapendi.

"Tunaomaba walimu hakikisheni mnaangalia vipaji walivyo navyo watoto wetu badala ya kuwalazimisha kusoma masomo ambayo hawayataki hali ambayo inaweza kuchangia kutofanya vizuri katika mitihani yao ya mwisho", alisema Dk. Isaya.

Kwa uapnde wake Mkurugenzi wa shule hiyo, Zefania Madaha alitaja hali ya nidhamu kwa watoto wanaohitimu shule hapo kuwa ni nzuri, huku akiwakumbusha wazazi na walezi kuendelea kuisimamia ipasavyo ili kuendeleza kizazi chenye nidhamu.

Alisema kuwa kuna mambo yamekuwa yakiuumiza katika jitihada nzima za kuwajengea wanafunzi maisha yao ya baadaye na kujua kuwa watakuwa katika viwanja gani wanapokuwa wakijenga maisha yao.

Naye Mkurugenzi wa shule hizo, Alexander Kazimiri alisema: "Kama wazazi sasa tunatakiwa kuhakikisha tunawajengea watoto wetu misingi ya maisha kupitia elimu, kwa kufanya hivyo hawatajutia kwani huo ndio urithi mkubwa katika maisha yao kuliko vitu vingine ambayo vipo hapa duniani".

# Tume Madini yajivunia masoko ya madini mikoani

Na Vitus Audax, MWANZA

TUME ya Madini imeendelea kutangaza fursa mbalimbali zinazopatikana katika sekta hiyo ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa masoko ya madini katika mikoa yote nchini.

Akitoa elimu ya upatikanaji wa leseni wakati wa Maonesho ya 18 ya Biashara Afrika Mashariki, Ofisa Madini kutoka Ofisi ya Madini Mkoa wa Mwanza, Adrian Anthony alisema kumekuwa na upotosha juu ya suala la upatikanaji wa leseni hizo kwamba ni mgumu na gharama.

Alisema hali hiyo inasababisha idadi kubwa ya wachimbaji kuacha kujishughulisha na ufatiliaji wa leseni hizo.

Kadhalika, alisema katika kuhakikisha jamii za wachimbaji madini zinaondokana na migogoro mbalimbali ikiwemo ya umiliki wa maeneo ya uchimbaji, Tume hiyo imeendelea kutoa elimu ya upatikanaji wa leseni za uchimbaji kwa wadau wa madini wa ndani na nje ya nchi.

"Niwaondolee hofu na dhana potofu wengi waliyokuwa nayo kuwa upatikanaji wa leseni ni kazi ngumu na inahitaji mtaji mkubwa sana kiasi kwamba Watanzania wachache wanaweza kumiliki leseni siyo, hivyo leseni zinapatika hadi kwa wachimbaji wadogo kwa kufuata utaratibu wa kisheria,"alisema Anthony.

Naye Ofisa Madini, Ratifa Mtamah alisema kuwa kupitia Tume ya Madini wanajitahidi kuhakikisha wanawafunulia Watanzania na wageni fursa zote zinazopatikana katika sekta hiyo, lengo likiwa ni kuhakikisha wanaongeza idadi ya wawekezaji wa ndani na nje kwa maendeleo ya taifa.

Ofisa Madini kutoka Ofisi ya Madini Mkoa wa Mwanza, Wilson Rwegasira alisema: "Tunapokea watu mbalimbali kutoka nchi tofauti za Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na wachimbaji wadogo, wakubwa pamoja na wanafuzi wanaohitaji kujifuza juu fursa katika sekta hii. Asilimia kubwa wanafurahi na elimu tunayowapatia".

Akifungua maonesho hayo, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exavery Kihage aliikumbusha Tume ya Madini kuhakikisha inatoa elimu kwa wazawa na kuwapa kipaumbele katika upatikanaji wa leseni na biashara ya madini lengo likiwa ni kuwasaidia kujiinua kiuchumi.

Alisema: "Wizara ya Madini pamoja na Tume ya Madini imekuwa ikifanya kazi kubwa ambayo imeongeza tija katika uchumi wa taifa ni suala muhimu kuhakikisha elimu inatolewa vyema na wazawa wanapewa kipaumbele katika upatikanaji leseni za uchimbaji".

Katika hatua nyingine tume hiyo ilipokea tuzo ya mtoa huduma bora katika kundi la watoa huduma wa taasisi za serikali na kuwa mshindi wa pili kwa kupata tuzo ya kombe pamoja na cheti kutoka kwenye Mamlaka ya TCCIA kwa kutambua mchango wake katika maonesho hayo yanayofanyika katika viwanja vya Furahisha jijini Mwanza.

# ama

ALHAMISI AGOSTI 31, 2023

AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 14

## Wanamazingira Afrika wanapokutana Kenya kuibua mapya kitisho tabianchi



## Kuendelea ukeketaji mabinti, wadau watajiwa 'kuvikwa mkanda wa mapesa' kichocheo kipya

Ukurasa 12

# Kahama ilivyo kiama kwa mama na mwana mabinti maelfu wateseka uzazi wa utotoni

• Wengi huzalishwa na waganga, wakunga mbumbumbu

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

UZAZI salama unajali suala la umri sahihi wa mwanamke kupata mtoto na pale anapojifungua chini ya miaka 18 inachukuliwa kuwa hatari kwa maisha ya mama na mwana, lakini Kahama mkoani Shinyanga mimba na uzazi utotoni ni kama vimekubalika japo ni kitisho kwa wanawake na watoto wao.

Wilayani Kahama ni kawaida kusikia taarifa za uzazi miongoni mwa watoto na kwa mwaka jana pekee mabinti 2,619 walijifungua, anaeleza Mratibu wa Mama na Mtoto wa Halmashauri ya Kahama Caroline Maliseli.

Aidha, kujifungua katika umri mdogo ni kuhatarisha usalama wa mjamzito na mtoto wake tumboni kwa sababu nyonga zinakuwa hazijafunguka, kadhalika wengi hawana uelewa juu ya kuhudhuria kliniki ili kujua maendeleo ya mtoto na kujifungulia nyumbani na kuzalishwa na watu wasiokuwa na utalaamu, anaonya mratibu huyo.

Anasema wimbi la wasichana wadogo kujifungua kabla ya wakati wao limekuwa kubwa na mwaka jana pekee jumla ya wasichana 2,619 walijifungua chini ya umri huo sawa na asilimia 16.

Anasema, mwaka huo wajawazito 17,605 walijifungua kati ya hao 2,619 walikuwa wasichana wenye umri chini ya miaka 20 na wengi wao ni wanafunzi wa shule za msingi na sekondari na tatizo la ndoa za utoto ni kubwa na linapaswa kutafutiwa ufumbuzi.



Mabinti wajawazito wakiteseka kujikimu hata kabla ya kujifungua. **PICHA: MTANDAO.**

Aidha, anasema, hao ni baadhi ya wanaofika katika vituo vya afya na kupata huduma, huku kundi kubwa likijifungulia majumbani na kufikia 497 sawa asilimia tatu na kuzalishwa na watu wasiokuwa wataalamu wa afya wakiwemo mama wakwe, waganga na wakunga wa jadi wote wakihatarisha maisha ya mama na mwana.

"Rika hili wakati wa kujifungua wanatumia pia dawa za kuongeza uchungu zinazowasababishia mfuko wa uzazi kupasuka na mtoto kunywa maji na kupoteza maisha, ofisini kuna chupa nyingi za dawa hizo na yote hayo wanayafanya kwa maelekezo ya mama wakwe. ,"anasema Caroline

**MATUKIO YA VIFO;**

Anaeleza kuwa mwaka 2021 mjamzito alizalishwa ndani ya duka la dawa na mhudumu katika Halmashauri ya Msalala, ambaye alitumia mbinu zilizosababisha mtoto kukatika kichwa, baada ya tukio hilo alitoweka na mama akabaki anatokwa na damu nyingi.

Caroline anasema mzazi alifikishwa hospitalini na kufanyiwa upasuaji kuondoa kichwa cha mtoto tumboni ambacho kilikuwa kikubwa na kwamba alikuwa hahudhurii kliniki kipindi cha ujauzito, licha ya kunusurika, alimpoteza mtoto.

Anawaonya kinamama kuacha tabia za kukwepa kliniki badala yake wanapopata uchungu wafike vituo vya afya na pia kuachana na tiba za asili ambazo ni hatari.

Kadhalika anasema,mwingine alikuwa mkazi wa kata ya Mhungula Manispaa ya Kahama alikuwa akizalishwa na mama mkwe wake baada ya kupata uchungu na mtoto alitanguliza miguu na walipomvuta walimkata kichwa pia, walimsaidia mama kwa kumfanyia upasuaji na kuondoa kichwa, na wote wanaozalishwa kwa njia za kienyeji wanapoteza vichanga vyao.

Anasema, pia katika kata ya Isagehe mjamzito mwenye umri chini ya mika 18 alipelekwa kwa mganga wa jadi na mama yake mzazi kuzalishwa kienyeji kwa kutumia vitu mbalimbali vilivyosababisha mtoto kubonyezwa fuvu la kichwa.

Walimfikisha hospitalini na kumsaidia hadi akajifungua salama lakini maumbile ya mazi yalivimba kutokana na kuchokonolewa na vitu ambavyo si salama, anaeleza Caroline.

**MAONI WANAJAMII**

Joseph Masanja, mwanafunzi wa kidato cha tatu Sekondari ya Nyikoboko anasema, kuna mwanafunzi mwenzao alipata ujauzito wakiwa kidato cha pili aliacha masomo hata kabla ya kufanya mtihani wa kuingia kidato cha tatu na alijifungua kwa njia ya upasuaji, mtoto yupo salama lakini mama yake alipata maradhi ambayo hakuyataja.

Katika Shule ya Msingi Shilela, Salumu Mashaka wa darasa la sita anasema, jirani yake alifaulu kujiunga na Sekondari ya Mwalimu Nyerere iliyopo Halmashauri ya Msalala, wazazi wake waligoma kumsomesha wakidai hawana fedha kumbe walitaka kumwozesha lakini walitoa taarifa polisi na mpango wao ukatibuliwa na sasa anaendelea na masomo.

Mkazi wa kata ya Kilago-Kahama Raphael Mazigwa, anasema,ili kukomesha ukatili kwa watoto hususani kuwaozesha kwa tamaa ya mali, ilihali wanahitaji kusoma ni vema jamii ikawa inaelezwa hatua zinazochukuliwa kwa wale wanaobainika kutenda vitendo hivyo ili ijue adhabu ambazo zimekuwa zikitolewa kwa watuhumiwa.

Aidha, anawashauri watendaji wa mitaa na kata kutojihusisha katika vitendo vya upatanishi pale mtoto au mwanafunzi anapopata ujauzito kwani wanamuachia majeraha moyoni mhanga hivyo wahakikishe mashauri wanayoyapata ofisni mwao wanayafikisha katika vyombo vya sheria kwa hatua zaidi.

Inaendelea Uk. 12

AFYA

# Kuendelea ukeketaji mabinti, wadau watajiwa 'kuvikwa mkanda wa mapesa' kichocheo kipya

**Na Sabato Kasika**

NI hivi karibuni wana mtandao wa kutokomeza ukeketaji wanakutana jijini Dar es Salaam, wakiibua mbinu mpya za kuhamasisha na kuendeleza ukeketaji wanawake na mabinti.

Wanaitaja kuwa ni mlengwa au binti kupewa 'mkanda' unaotengenezwa na pesa kuanzia noti za Shilingi 2, 000 hadi 10,000 zinazobanwa na pini akivalishwa mabegani na zinazoongezeka kila anapokuja yeyote kumtunza hivyo kuondoka na mamilioni.

Anavalishwa mkanda kuanzia mabegani hadi chini ukiwa umejaa fedha hizo mpya anazopokea mara baada ya kukeketwa, anasema Mary Mwita, mmoja wa walioathirika na mbinu hiyo.

Anaongeza kuwa na mamilioni shingoni hadi chini miguuni kunawavuta wasichana ambao bila shaka wataona ukikeketwa unatajirika.

Anasema ikitokea aliyekeketwa akafariki, anazikwa na fedha hizo, kwa imani kwamba huo ni mkosi, wazazi au walezi hawawezi kuzichukua.

Mary ni mmoja wa waliopitia mateso hayo, anayeweka wazi siri hiyo na kufafanua kuwa inachangia kuwafanya mabinti kuvutiwa na mtego huo unawawapeleka kukeketwa.

"Zipo mbinu nyingi zinazofanyika katika kufanikisha ukeketaji, lakini hii ya kuwatuza fedha wakeketwaji imeshamiri, kwa kuwa wanajua hawawezi kuzikataa, ndiyo maana ukeketaji unaendelea," anasema Mary.

Mary anazungumza kwenye mkutano wa wadau unaofanyika Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, akitoa elimu kuhusu ukatili wa kijinsia na masuala ya afya ya uzazi ngazi ya jamii.



Mary Mwita akielezea mbinu zinazotumika kuendeleza ukeketaji. **PICHA: SABATO KASIKA**

Mhamasishaji huyo wa mtaa wa Kerezange, anasema anatambua jitihada zinazofanywa na wadau kukomesha ukeketeji, lakini anaomba jamii ijue kuwa mtindo wa kuwatuza fedha wanaokeketwa, unachangia kuwapo kwa vitendo hivyo.

"Kikao cha wadau wa mtandao kupinga ukeketaji kufanyika Kipunguni ni sahihi, kwani inaoongoza kwa ukeketaji jijini Dar es Salaam, wakeketaji wanafanya bila kificho," anasema.

Aidha, anasikitishwa kuona baadhi ya watu kwenye jiji hilo kitovu cha biashara na uchumi mkubwa, wakitembea na visu , marungu na bakora hadharani kuashiria kuwa tayari wapo mabinti wanatoka kukeketwa.

Mila hiyo ya Kikurya inatumika kuonyesha kuwa ukeketaji umekamilika wakishangilia na kuenzi utamaduni huo.

### WADAU WAAZIMIA

Katika kikao hicho, wadau hao ambao baadhi yao ni wanachama kutoka mikoa mbalimbali wapo wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ( (LHRC), Himiza Development Organization, Gai Tanzania na Vision for Future Life, wanaazimia kutoa elimu ya kukataza ukeketaji kwa bidii zaidi.

Mwenyekiti wa Mtandao Kutokomeza Ukatili Tanzania, Roman Selesini, anasema watazingatia kuelimisha jamii madhara ya ukeketaji, ili watu wawe na uelewa wa kutosha.

"Ninatambua juhudi za wadau katika vita hii, lakini ipo haja ya kuongeza kasi ya vita hii, kwani wote tunajua ukeketaji ni hatari kwa afya ya mtoto wa kike," anasema Selasini.

Anaamini elimu dhidi ya vitendo vya ukeketeji ikitolewa kikamilifu licha ya baadhi ya wazazi na walezi kuwa wagumu na kukumbatia mila na desturi zilizopitwa na wakati, mambo yatabadilika.

Halikadhalika anakumbusha kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wahusika, huku akiungwa mkono na John Simwanza wa LHRC anayesema umefika wakati wa kuweka sheria kali, ili wanaoendekeza vitendo hivyo wachukuliwe hatua haraka, liwe fundisho kwao na kwa wengine wanaofanya hivyo.

"Sheria kali zinaweza kuwagopesha na kuachana na mtindo ambao sasa tunaelezwa hjapa kwamba wameanza kukeketa bila kificho. Hii haifai hakuna anayeweza kukubali," anasema Simwanza.

Anaongeza kuwa mifumo ya utoaji wa taarifa na utekelezwaji nao uwe rafiki kwa pande zote ili kuharakisha vita hiyo ya ukeketeji katika eneo hilo na nchi nzima hasa maeneo ambayo kuna vitendo hivyo.

Diwani wa Viti Maalum Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, Fatuma Kingwande, anasema viongozi wa serikali na chama wanapiga vita vitendo hivyo, na kwamba wadau waendelee kuungwa mkono.

Mkuu Msaidizi wa kituo kidogo cha polisi Kitunda, Peter Mwankusi, anaahidi kuwasilisha maazimio ya wadau hao, kwa kwa wakuu wake wa kazi kwa utekelezaji.

### HALI YA UKEKETAJI

Katika taarifa yake ya hivi karibuni, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Dk. Dorothy Gwajima, anasema vitendo hivyo ni tatizo kubwa.

Anasema hayo wakati akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ukeketaji dhidi ya Wanawake na Watoto wa kike Duniani, jijini Dodoma.

Anafafanua kuwa serikali kwa kushirikiana na wadau, inaendelea na jitihada za kukabiliana na vitendo vya ukeketaji kupitia mipango na mikakati iliyowekwa, ikiwamo kutunga na kufanya marekebisho ya sheria na sera mbalimbali za nchi.

Wakati akisema hayo, Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Watoto Sehemu ya Familia wa wizara hiyo, Asha Shame, anasema Tanzania ina asilimia 10 ya vitendo vya ukeketaji, huku akitaja mikoa inayoongoza kwa ukeketaji kuwa ni Manyara asilimia 58, Dodoma asilimia 47, Arusha asilimia 41, Mara asilimia 32 na Singida asilimia 31.

## KAHAMA ILIVYO KIAMA KWA MAMA NA MWANA MABINTI MAELFU WATESEKA UZAZI WA UTOTONI

INATOKA UK. 11

### USTAWI WA JAMII.

Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Manispaa ya Kahama Swaiba Chemchem, anasema, ukatili wa kijinsia kwa watoto wenye umri chini ya miaka 18 bado upo na unatakiwa kudhibitiwa ili kuwapa nafasi ya kutimiza ndoto zao za kielimu.

Anasema, watoto 881 wamefanyiwa vitendo mbalimbali vya ukatili na unyanyasaji kwa kipindi chama miezi tisa mfululizo mwaka jana.

Aidha, anasema, kati ya hao 255 walikuwa wa kiume na 469 wa kike na vitendo hivyo vimekuwa vinafanywa na watu wanaoishi nao na kuwaamini tena wanaojua kuwa ni kosa kisheria na wanapobainika wamekuwa wakishtakiwa kwa mujibu wa sheria ya mtoto namba 21 ya mwaka 20019.

Swaiba anasema, kati ya hao ndoa za utotoni zilikuwa 11, mimba za utotoni 31 kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, kutupa watoto matukio saba, ajira za utotoni 14 na usafirishaji haramu wa watu kutoka sehemu moja hadi nyingine ilikuwa mikasa 101 na kuwaomba wazazi na walezi kushirikiana pamoja kutokomeza vitendo hivyo.

"Utoaji wa elimu ya ukatili na madhara yake kwa kushirikiana na mashirika ya kiraia yanayofanya kazi na serikali ikiwemo SHDEPHA+ imewaibua wananchi kujitokeza na kutoa taarifa na kuwanusuru watoto wanaozeshwa wakiwa bado shuleni, na bado tunaendelea kuchukua hatua pale tunapobaini wazazi kuhusika moja kwa moja,"anasema Swaiba.

### UBAKAJI WAONGEZEKA

Mwenyekiti wa Asasi ya Wanawake 100,000 mkoani Shinyanga, Anascholastica Ndagiwe, anasema, wanafunzi au wasichana wanaopata ujauzito wengi wanabakwa na hivi karibuni alibakwa mwanafunzi wa darasa la nne na mshitakiwa kuhukumiwa miaka 35 jela licha ya hukumu kutolewa akiwa nje kwa dhamana, na hata sasa hajulikani alipo.

Anasema pia baadhi ya wazazi na walezi wamekuwa chanzo cha watoto wao kupata ujauzito wakiwa shuleni na familia nyingi wanatelekeza watoto na mabinti wakilazimika kuwalea wadogo zao na hii inasababisha kuingia kwenye ngono wakiwa na umri mdogo ili kupata fedha za kujikimu.

John Banda, Mwalimu wa Taalumu wa Sekondari ya Nyikoboko anakiri kuwepo kwa tatizo la wanafunzi wa kike kupata ujauzitio na kushindwa kuendelea na masomo na kwamba wanakuwa na uwezo mkubwa darasani na mwaka 2022 kuliripotiwa kesi moja ya mwanafunzi wa kidato cha tatu kupata ujauzito. Halikadhalika anasema, kuna mwanafunzi alifanya mtihani akiwa na ujauzito bila wao kujua na alifaulu kuingia kidato cha tatu lakini alishindwa kuendelea na masomo kwa sababu ya mimba na vitendo hivyo vya kikatili vinafanyika ndani ya jamii wanazotoka na baadhi ya wazazi na walezi ni watuhumiwa moja kwa moja.

Joseph Samwel kutoka kituo cha Taarifa na Maarifa kata ya Shilela wilayani Kahama anasema, kila mwezi wamekuwa na utaratibu wa kutembelea kijiji kimoja na kutoa elimu ya madhara ya ndoa na mimba za utotoni na zile wanazozibaini wanaziripoti katika vyombo vya sheria kwa hatua zaidi.

AFYA

# BMH inavyokabili ugumba, ukosefu wa nguvu za kiume

## • Matumaini, heshima iliyopotea yarejea tena kwa kinababa

**Na Christina Mwakangale, aliyekuwa MBEYA**

KUNA wakati maisha hupitia changamoto kadhaa ziwe kiafya, uchumi na hata uzazi, John Bryson, kuishi bila ya kuwa na nguvu za kiume na kushindwa tendo la ndoa ni mambo yanayomtatiza.

Kijana huyo mkazi wa Mbeya Mjini, amekata tamaa na kuamua kulewa muda wote, ndivyo anavyosimulia maisha yake kwa Nipashe, akisema amekabiliwa na tatizo la kukosa nguvu hizo kwa miaka kadhaa.

Tatizo lake limepata tiba, ni wakati huu wanaume wanaokumbwa na shida hiyo, wanapokutana na usaidizi wa kitaalamu wa kupandikizwa visisimua uume.

Habari njema ilisikika Juni 14 mwaka huu katika Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH), Dodoma, hapo wataalamu wa Chama cha Madaktari Bingwa wa Upasuaji Mfumo wa Mkojo Tanzania (TAUS) na mbobezi kutoka Ufaransa, wanashirikiana kuanzisha teknolojia hiyo.

Dokta Remigius Rugakingira mbobezi wa magonjwa ya mfumo wa mkojo na wanaume (urolojia) wa BMH akizungumzia tatizo hilo, anasema wameamu kuja na suluhisho hilo baada ya kubaini kuna shida miongoni mwa wanaume wakilenga kusaidia ambao uume unakosa nguvu na kuwarejeshea faraja kinababa hao waliokosa watoto.



John akizungumza na mwandishi wa taarifa.

**MAISHA YA JOHN**

John mkazi wa Nzovwe mjini Mbeya, anayaona maisha ni magumu kwake, akisema anaishi bila kuwa na mwenza na kwamba hakutarajia pia kupata mtoto.

Anasema alibaini kuwa ana tatizo hilo akiwa na umri wa miaka 20 na kwamba hakikuwa kikwazo kwake kwa kuwa alikuwa mwanafunzi wa kidato cha nne.

"Nilidhani kwamba bado ni mdogo. Maana wakubwa wanatuambia tusome shule kwanza tukimaliza tutayakuta mambo ya kikubwa. Ajabu nimeishi hivyo hadi sasa, uume wangu si kama wa wengine...natamani kuwa na familia ila nawaza kuoa kutakuwa mwanzo wa aibu yangu kuwekwa hadharani," anaeleza John.

Anasema kwake faraja ni kushinda vijiweni kuzungumza na vijana wenzie na ikifika saa 12 jioni huhamishia furaha yake kwenye vilabu vya pombe, akirejea nyumbani kwake ni usiku wa manane.

"Siku yangu naifanya iwe fupi, napiga stori na washkaji mchana ila jioni nahamia kilabuni. Natamani kupata tiba kama ipo. Kwa sababu nimetumia za kienyeji nimeshindwa. Ingawa nimesikia kupitia taarifa za habari, kuna huduma ya kututibu watu kama sisi. Lakini najiuliza nitamudu gharama, sina kazi yenye ujira rasmi, nafanya vibarua hasa kubeba mizigo, kwa siku naingiza Sh. 2,000 hadi 2,500," anasema John.

Kwa mujibu wa tovuti ya 'edtreatmentindia', upandikizaji huo nchini India hugharimu Dola za Marekani 6,000 hadi 10,000 huku huduma kama hiyo Uingereza au Marekani ikifikia kati ya Dola 15,000 hadi 25,000.

**KILICHOISUKUMA TAUS**

Daktari Rugakingira, anasema TAUS, katika mkutano wake wa pili tangu kuanzishwa uliofanyika Dodoma, mwaka huu, moja ya ajenda ilikuwa ni kupata suluhisho kwa wanaume wenye tatizo la nguvu za kiume.

> **"Najiona vyema kuwa mmoja wa walioanzisha huduma kupandikiza uume, nakumbuka pia nilikuwa katika jopo la waanzilishi wa kupandikiza figo najua wengi wanafanya makubwa kama mimi.**

"Tuliona umuhimu wa kuanzishwa huduma hii. Kazi yetu kubwa ni kutibu nguvu za kiume, kuanzisha huduma hii ambayo watu walikuwa wanaipata nje kwa gharama kubwa.

"Huduma hii ipo Afrika katika nchi chache, nasi tumekuwa wa kwanza. Upandikizaji huu usifananishwe na kupandikiza uume wote. Mfano nina mwalimu wangu Afrika Kusini, alishampandikiza mgonjwa uume baada ya mgonjwa aliyekufa ubongo kuamua kutoa uume wake kabla hajafa," anaongeza;

Anasema baada ya hospitali hiyo kuanzisha huduma hiyo, mwitikio na maswali kutoka kwa wanajamii kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, umekuwa mkubwa huku zaidi ya watu 40,000 wakiuliza huduma hiyo.

"Tumebaini wengi wana tatizo na hawana elimu kuhusu nguvu za kiume. Sio kila anayepata shida hiyo suluhisho linakuwa moja, yapo mengi. Na hii huduma ni mojawapo, ingawa kuna dawa na ushauri.

Anasema pamoja na huduma hiyo kufika nchini, zipo changamoto ikiwamo upatikani wa vipandikizi ambavyo hutumika ili kuuongezea uume nguvu,

"Kinachotakiwa ni vifaa na vipandikizi, changamoto itakuwa vifaa na gharama, ila serikali ina wataalamu na itaamua namna ya kupanga gharama ili kuhudumia watu.

Anawaalika wenye changamoto hizo kufika hospitalini na kinamama pia ambao wanapitia shida ya uzazi, lakini hawapati watoto hilo ni suluhisho kwao akisema asilimia 60 hadi 80 wengine wana tatizo la kisaikolojia wakishauriwa wanarudi katika hali zao kama kawaida.

"Iwe chachu kwa wanataalama wenzetu kukiri kwamba tunaweza, tupende vya kwetu. Lakini inatupa fursa hasa wawekezaji wa viwandani kwa sekta ya afya, wakawa na vifaa yaani vipandikizi, vikipatikana hapa nchini wengi watatibiwa na kuifanya nchi yetu kuwa kituo cha kufanyia utalii wa afya."

Bingwa huyo anasema, upandikizaji huo hutumia saa mbili kwanza huanza kwa ushauri kwa mgonjwa, kabla ya kufanyiwa upasuaji na baada ya hapo mgonjwa huyo huhitajika kufanyiwa ufuatiliaji kwa miezi kadhaa, ili kujua maendeleo yake.

"Najiona vyema kuwa mmoja wa walioanzisha huduma kupandikiza uume, nakumbuka pia nilikuwa katika jopo la waanzilishi wa kupandikiza figo najua wengi wanafanya makubwa kama mimi.

Anaeleza kuwa kwa siku wanaweza kupandikiza wanaume wanne kulingana na uhitaji, wakiangalia pia sifa na vigezo kwa ambaye anaweza kufanyiwa huduma hiyo. Kiongozi wa TAUS, Dk Lyuba Nyamsogoro, anasema kuwa wamefikia hatua hiyo kutokana na uwepo wa watu wengi wenye matatizo ya nguvu za kiume nchini na Afrika kwa ujumla.

"Mojawapo ya dhumuni la TAUS ni kuendeleza wataalam nchini kwa kushirikiana na wabobezi wengine kutoka nje ili kuiletea Tanzania teknolojia inayopatikana duniani na kutibu wagonjwa wenye matatizo," anasema Dk Nyamsogoro.

Msemaji wa BMH Jeremiah Mbwambo, anaeleza, kuwa hospitali hiyo inakuwa ya kwanza nchini kufanya upasuaji wa kuweka vipandikizi kwenye uume kwa wagonjwa wenye matatizo ya nguvu za kiume na kwamba serikali inaendelea kufanya uwekezaji kwa kuwawezesha teknolojia za kisasa za matibabu.

MAZINGIRA

# Wanamazingira Afrika wanapokutana Kenya kuibua mapya kitisho tabianchi



Maelfu ya wanyama hufa Afrika kutokana na ukame . **PICHA: BBC**

**Na Mwandishi Wetu**

MKUTANO wa hali ya hewa au wa mabadiliko ya tabianchi barani Afrika, unaanza Jumatatu ijayo jijini Nairobi. Likiwa ni jukwaa la kushughulikia ongezeko la changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa na gharama zinazohusiana na tatizo hilo kote duniani lakini pia hasa barani Afrika.

Ni mkutano unaotarajiwa kueleza wapi Afrika ilipo na inapokwenda, hatua za haraka zinazohitajika kuchukuliwa ili kupunguza changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa, unaeleza mtandao wa Mtandao wa africaclimate.org.

Septemba 4 hadi 8 ndiyo siku za mkutano huo ambao pia unapewa jina la Africa Climate Week 2023 au Wiki ya Hali ya Hewa barani Afrika.

Ni juma linalotoa fursa kwa watunga sera, watendaji, wafanyabiashara, na mashirika ya kiraia kubadilishana taarifa kuhusu changamoto na ufumbuzi wa masuala ya hali ya hewa, vikwazo vya kukabili na fursa zinazopatikana katika maeneo mbalimbali.

Wiki ya Hali ya Hewa barani Afrika itajielekeza kwenye maeneo manne kwa nia ya kutoa michango inayolenga kupata mambo au ajenda ambazo kanda ya Afrika itafikisha kwenye jukwaa la kimataifa la mkutano wa mabadiliko ya tabianchi wa kikao cha 28 cha Mkutano wa Nchi Wanachama COP 28 kitakachofanyika kuanzia Novemba hadi Desemba 12, 2023 huko Umoja wa Falme za Kiarabu.

Mambo ambayo washiriki wa wiki hiyo ya Afrika watayajadili kwa kina ni pamoja na nishati na viwanda, majiji, miji na makazi mijini. Aidha, suala jingine ni miundombinu, usafirishaji na usafiri.

Kadhalika watajadili ardhi, bahari, vyakula maji, jamii pamoja na afya, kupata mahitaji muhimu kama maji, chakula, dawa, makazi na mavazi (livelihoods) na uchumi, kwa mujibu wa wa africaclimate.org

### MAMBO YALIVYOANZA

Masula ya tabianchi yamenza kushughulikiwa takribani miaka 31 iliyopita, ilikuwa 1992 mkutano wa kwanza wa wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN), ukifanyika jijini Rio de Jenairo nchini Brazil.

Miongoni mwa mashuhuda wa mchakato huo ni Mkurugenzi mstaafu wa Idara ya Misitu na Nyuki nchini, Dk Felician Kilahama, anayesema katika mahojiano kuwa ni miongo mitatu tangu mambo ya mabadiliko ya tabia nchi yalipoanza, lakini halipo la kujivunia kwani hakuna hatua za kuridhisha zilizopigwa. Anakumbusha kuwa mkutano wa kwanza wa masuala hayo wa Rio uliunda chombo kiitwacho United Nations Framework Convention on Climate Change (UNFCCC).

Jopo hilo la Umoja wa Mataifa la UNFCCC linaundwa na watu mbalimbali wakiwamo wataalamu,wanasayansi mashuhuri,wakuu wa nchi, wasomi , watafiti na asasi za kiraia wamekuwa wakikutana kila mwaka, waanza kwanza wataalaam kuandaa masuala ambayo Wakuu wa nchi wataweza kukubaliana na kuyapitisha, ukifanyika kwa wiki mbili kati ya Novemba na Decemba kila mwaka.

Wakuu wa nchi kushiriki kikao hicho siku tatu za mwisho na huitwa (High-level Session), wakifanya maamuzi, baada ya kuchakatwa na wataalam mbalimbali wa sayansi na mazingira, anaongeza mtaalamu huyo. Mambo ambayo wakuu wa nchi waliwahi kufanyia maamuzi ni kuundwa kwa mifuko kadhaa ya kushughulikia tabianchi. Moja wapo ni 'Adaptation Fund' au mfuko wa uhimilivu, mwingine ni wa fidia ya maafa na ule wa Global Environment Facility (GEF).

Adaptation Fund husaidia nchi wanachama kuweza kukabiliana na majanga yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi, anaeleza Dk.Kilahama.

Aidha, ni pamoja na kuimarisha uwezo wa kukabiliana na matatizo kama kilimo cha uhimilivu kutokana na ukame, kuzuia mmomonyoko wa udongo, kukabiliana na mafuriko, kuongeza uwezo wa nchi kuwa na misitu ya kutosha kama mbinu halisi ya kuondoa mlundikano wa gesiukaa hewani na kuongeza zaidi oksijeni.

### BIASHARA YA GESI

Hapa kuna mkakati wa kuweza kufanya biashara ya gesiukaa (carbon trading), akizungumzia biashara hiyo Dk. Kilahama anasema kwa uzoefu wake, kumekuwa na maneno ya mengi kukabiliana na matatizo yanayotajwa lakini vitendo hakuna kinachoridhisha hata kidogo.

"Ni siasa zaidi kuliko kuchukua hatua. Kiuhalisia mataifa yaliyoendelea, nchi tajiri ndiyo wazalishaji wa kiasi kikubwa cha gesiukaa ukilinganisha na mataifa yanayoendelea kama Tanzania. Kikwazo kwa mataifa makubwa kuchukua hatua ni "uchumi" viwanda vyao kuweza kurekebisha vyanzo vya nishati ni changamoto kubwa na hawako tayari kuona mapato ya nchi yanashuka sana. Hivyo suala la mabadiliko ya tabia nchi ndani ya miaka 31 iliyopita halijaweza kuzaa matunda na mambo ya kujivunia." Anasema

Kadhalika, mifuko ipo na fedha wanaweka lakini siyo kama wanavyokubaliana na nchi maskini na zinazoendelea kuweza kupata fedha hizo nayo ni changamoto nyingine. Kuna mikwara mingi na michakato ya kitaalamu ni mirefu kiasi kwamba uwezo wa nchi zenye uchumi unaoinukia ni mdogo, anasema mtaalamu huyo.

Anaongeza: " Ukiangalia masuala ya kufanya biashara ya gesiukaa, siyo rahisi kama ilivyokuwa ikionekana katika kikao cha Desemba, 2007 kilichofanyika Bali nchini Indonesia. Kikao hicho kilikuwa kimenipa matumaini makubwa na nikaona iwapo mambo yatakuwa kama yalivyozungumzwa, misitu katika nchi za Afrika, itapona maana nilitegemea wananchi watawezeshwa na hatimaye waweze kuitunza misitu ya asili na kupanda miti mingi zaidi katika maeneo yao kwaajili ya kuuza gesiukaa na kupata fedha."

Anasema kuwa matokeo yake hadi sasa hakuna matumaini makubwa ingawa kuna maelezo kuwa michakato inaendelea, na kwamba wakati anastaafu 2012 hadi sasa (zaidi ya miaka 10) hakujawa na uhakika biashara ya gesi ukaa inakuwaje?

Dkt. Kilahama anasema imekuwa ni kuhangaika na wakati huo kasi ya kutoweka misitu ya asili nchini ikiwa ni kubwa, hali hiyo ni tishio kwa uhai wa mazingira na maendeleo ya taifa kwa ujumla.

Anasema angalau kwa mashamba ya miti Tanzania imejitahidi kupitia Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), lakini kwa misitu ya asili usimamizi wake ni kidogo mno , hata hivyo, kwenye ile ya lindimaji au misitu hifadhi asilia (nature forest reserves), imekuwa ikilindwa na kuendelezwa kwa msaada wa mfuko wa The Global Environment Facility (GEF) kupitia Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP) kwa kushirikiana na serikali kupitia TFS, Wizara ya Maliasili na Utalii.

### AHADI TATA

Katika Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Hali ya Hewa wa 2009 au Mkutano wa Copenhagen, uliofanyika Copenhagen, Denmark ukipewa jina la COP15 mwaka 2009, nchi zilizoendelea ziliahidi kwa pamoja kuhamasisha kupata dola bilioni 100 ifikapo 2020 kusaidia hatua za hali ya hewa katika nchi zinazoendelea.

Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa za UN lengo hilo halijafikiwa kama ilivyokuwa imekusudiwa na juhudi zinaendelea. Kama ndivyo hali ilivyo kazi ni ngumu na ufumbuzi huenda ukawa vigumu kupatikana, kwa vile waongeza joto na mabadiliko ya tabianchi hawako tayari kuwajibika.





## Kongamano kujadili uwekezaji bandari kufanyika Oktoba

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHUJAA wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii Tanzania (SMAUJATA) Mkoa wa Singida wanatarajia kufanya kongamano la kujadili mambo mbalimbali ikiwamo uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam na ukatili wa kijinsia.

Kamati ya maandalizi ya kongamano hilo wakiongonzwa na Mwenyekiti wa SMAUJATA Mkoa wa Singida, Dismas Kombe, waliwaeleza jana viongozi wa Wilaya ya Ikungi walipokutana kwa ajili ya kuomba michango ya Sh.milioni 11.5 kwa ajili ya kufanikisha tukio hilo.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Juma Amrani alisema kongamano hilo litafanyika Oktoba 7, 2023 katika stendi ya mabasi ya zamani mjini Singida.

Alisema wakati wa kongamano hilo shughuli zitakazofanyika ni kutoa elimu ya vitendo vya ukatili wa kijinsia, uchangiaji wa damu salama, elimu kuhusu mkataba wa Bandari ya Dar es Salaam, Dira ya Maendeleo ya Taifa kuanzia mwaka 2025/2050.

Amrani alitaja mambo mengine yatakayokuwepo kwenye kongamano hilo kuwa ni elimu salama mashuleni hasa kwa mtoto wa kike na kupunguza alama sifuri, kwamba watakuwepo wataalamu mbalimbali wakiwemo maafisa ustawi wa jamii na maendeleo ambao ndio watatoa mada.

Naye Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Omari Mwangi, alisema wanaamini kupitia kongamano hilo jamii itapata elimu ya kupunguza kama siyo kumaliza vitendo vya ukatili vilivyokithiri mkoani hapa kutokana na mmomonyoko wa maadili ambapo kwa upande mwingine kunachangiwa na wazazi au walezi.

''Wazazi wengi wamekuwa wakikwepa majukumu ya malezi ya watoto wao na kuwaacha wafanye mambo yao jambo ambalo limewafanya wajikute wakiingia katika makundi yasiofaa na kuanza kufanya vitendo vilivyo kinyume na maadili,'' alisema.

Makamu Mwenyekiti wa SMAUJATA Mkoa wa Singida, Ambwene Kajula, alisema kuwa lengo la kongamano hilo ni kuwapata viongozi ili wapate majibu ya moja kwa moja kutokana na kero mbalimbali walizonazo wananchi dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Alisema pamoja na jitihada kubwa inayofanywa na SMAUJATA ya kupambana na vitendo vya ukatili bado elimu haijawafikia watu wengi na kupitia kongamano hilo wataweza kuipata kupitia michezo ya kuigiza na kutakuwa na makala maalumu ya video.

# Kairuki atoa maagizo shuleni kuhusu chakula

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ALIYEKUWA Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Angellah Kairuki, ameagiza shule zote za umma na binafsi nchini kutekeleza mwongozo wa utoaji chakula shuleni.

Aidha, amewataka wazabuni wote waliopewa zabuni za kuhudumia vyakula katika shule kuongeza virutubisho kwenye unga unaotumiwa, huku akipiga marufuku matumizi ya chumvi ambazo hazina madini joto kwa wanafunzi.

**Katika kutekeleza hili, Rais Samia aliniagiza kusimamia zoezi la kufanya tathmini ya haraka kwa kushirikiana na Shirika la Big Win Philathropy la Marekani ili kubaini visababishi vikuu vya utapiamlo nchini.**

Kairuki, alisema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akifungua mkutano wa mwaka wa tathimini ya saba ya mkataba wa lishe nchini.

Alisema Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itaendelea kusimamia utolewaji wa afua za lishe kwa kusimamia mikoa pamoja na halmashauri katika utekelezaji wa mkataba huo.

"Katika kufanikisha utekelezaji wa afua za lishe nchini shule zote za umma na binafsi zinapaswa kutekekeleza mwongozo wa shule kutoa chakula shuleni na wazabuni wanaopewa kazi za kuhudumia chakula wahakikishe kuwa wanaongeza virutubisho katika vyakula vinavyotumiwa na wanafunzi shuleni na ni marufuku matumizi ya chumvi zisizokuwa na madini joto" alisema Kairuki.

Aidha, aliwataka wakuu wa mikoa kusimamia afua za lishe na fedha zilizotengwa zinatolewa kwa wakati na kutumika katika matumizi yaliyopagwa.

"Wakurugenzi wa halmashauri pia mhakikishe kuwa fedha za lishe zinafanya kazi kwa malengo yaliyokusudiwa na ni marufuku kutumia fedha za OC za idara ya afya au idara nyingine kwakua suala la lishe ni jambo muhimu sana hivyo ni marufuku kuanzia leo kutumia fedha za OC kwa ajili ya utelezaji wa afua za lishe" alisema

Kadhalika, alisema kwa kutambua umuhimu wa lishe bora na madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na upungufu wa lishe, serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikichukua hatua za kukabiliana na utapiamlo nchini.

Alisema juhudi hizo ni pamoja na kuwa na mpango jumuishi wa utekelezaji wa masuala ya lishe kitaifa ulioainisha afua zote muhimu zinazopaswa kutekelezwa na sekta na wadau mbalimbali nchini.

"Aidha, serikali imekusudia kuimarisha utafiti za lishe nchini ili kutambua kwa kina visababishi vya lishe duni ili mikakati madhubuti iweze kuwekwa katika kuondoa visababishi hivyo.

"Katika kutekeleza hili, Rais Samia aliniagiza kusimamia zoezi la kufanya tathmini ya haraka kwa kushirikiana na Shirika la Big Win Philathropy la Marekani ili kubaini visababishi vikuu vya utapiamlo nchini," alisema.

Alisema tayari tathmini hiyo imeshafanyika na sasa wapo katika hatua za mwisho za uandaaji wa taarifa ambayo itawasilishwa kwa Rais hivi karibuni.

Alisema taarifa hiyo itawasaidia kujua visababishi vya utapiamlo katika maeneo tofauti ya nchi na kutoa mwelekeo wa aina ya afua zinazotakiwa kutekelezwa katika maeneo hayo ili kuleta matokeo chanya na ya haraka na endelevu.

Alisema utafiti huo ulifanyika katika mikoa sita ya Njombe, Tabora, Geita, Dar es Salaam, Mtwara na Iringa kwa Tanzania Bara na mikoa miwili ya Tanzania Visiwani.

Alisema tafiti zinazohusu lishe zilizofanyika nchini zinaonyesha kuwa na uelewa mdogo wa masuala ya lishe katika jamii, kuanzia ngazi ya familia hadi kwa watendaji na viongozi wa serikali ni moja ya changamoto kubwa katika juhudi za kukabiliana na utapiamlo hapa nchini.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dk. Willson Mahera alisema moja ya tatizo katika utekelezaji wa afua za lishe nchini ni mitazamo kwa wananchi hususani katika ulaji wa vyakula.

Alisema: "Katika nchi za wenzetu mtu ukisema unakula wali samaki hivyo lazima samaki awe mkubwa kuliko wali au ugali nyama lazima nyama ziwe nyingi kuliko ugali kwakua protini ndiyo lishe lakini ugali ni wanga tuu kwa ajili ya kuongeza nguvu mwilini, hivyo tunapaswa kubadili mitizamo yetu" alisema.



Ofisa Miradi Msaidizi wa Uboreshaji wa huduma za mama na mtoto, Dk. Hamoud Ndege akizungumza na washiriki kutoka TAMISEMI, Wizara ya Afya Zanzibar na Tanzania Bara, mashirika yasiyo ya kiserikali na wafadhili wa kutoka nchi ya Italia, wakati wa uzinduzi wa huduma hiyo, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# 'Mchwa' fedha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wapewa onyo

**Na Elisante John,** SINGIDA

SERIKALI imeutaka Mfuko wa Maendeleo ya Jamii nchini (TASAF), kusimamia kwa karibu fedha za ruzuku zinazotolewa kwa ajili ya kaya masikini vinginevyo watumishi watakaojihusisha na ufisadi watapoteza ajira kwa ukiukwaji wa taratibu za malipo.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, Ridhiwan Kikwete, alisema hayo juzi alipofanya ziara mkoani Singida, kujionea shughuli mbalimbali zinatekelezwa na TASAF.

Kikwete, alisema hayo alipojionea shughuli za walengwa wanaohudumiwa na mfuko huo, wakiwemo wa ufugaji mbuzi, kondoo na kuku wa asili, katika Kijiji cha Ughaugha, kilichopo Manispaa ya Singida.

"Niwaombe sana waratibu wa TASAF kote nchini, mnaofanya kazi kwenye Halmashauri ya Wilaya, Manispaa na Jiji, simamieni malipo halisi, sikilizeni kero na tatueni changamoto zao za malipo...utapoteza ajira na nisingependa hili likutokee," alifafanua Kikwete.

Alisema serikali katika mwaka huu wa fedha imetenga zaidi ya Sh. bilioni 51 kwa ajili ya malipo ya ruzuku, hivyo ni jukumu la walengwa kuzitumia fedha hizo kwa malengo yaliyokusudiwa.

Baadhi ya walengwa wa mfuko huo wa Kijiji cha Ughaugha B, Manispaa ya Singida, Elizabeth Joseph na Jaquleen Shabani, waliishuruku serikali, kwa kuyaboresha maisha yao tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

"Tunaishukuru sana TASAF, imeniwezesha maisha mazuri, sasa nafuga mbuzi watatu, kuku na watoto angu sita wanakwenda shule wanaendelea vizuri na masomo... asanteni sana na Mungu awabariki," alisema.

Mratibu wa TASAF, Stara Beka, alisema pamoja na mafanikio ya mfuko huo katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida, bado kuna mahitaji ya wananchi wengi kuomba waingizwe kwenye mpango wa kunusuru kaya maskini.



# Mgombea ubunge aahidi kutatua mgogoro

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

MGOMBEA ubunge wa Mbarali mkoani Mbeya (CCM), Bahati Ndingo ameanza kampeni za kuwania nafasi hiyo, huku mgogoro wa mpaka kati ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na wananchi ukitawala kwenye ajenda zake.

Akiwa katika kampeni, Bahati alisema hawezi kuwaahidi wananchi kwamba atatatua mgogoro huo bali atakuwa daraja kati ya wananchi na serikali katika kutatua mgogoro huo ambao umekuwa ukisababishwa na Tangazo la Serikali Namba 28 (NG.28) la Mwaka 2008.

Akizungumza na wananchi wa Kata ya Madibira, alisema atahakikisha anashirikiana na wananchi hao kufanya mazungumzo na serikali ili mipaka hiyo irekebishwe.

**Wakala wa Barabara nchini (TANROAD) wamejenga daraja katika eneo hilo na limekamilika kwa muda mrefu lakini bado halijafunguliwa jambo ambalo linakwamisha shughuli zao.**

Alisema maeneo ya wananchi yaliyochukuliwa kwa ajili ya kupanua mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ni makubwa na hivyo wengi wamekosa maeneo ya kulima, kuishi na hata kuchungia mifugo yao.

Alisema tatizo hilo limekuwa kikwazo cha uchumi wa wananchi wa maeneo hayo ambao shughuli zao kubwa ni kilimo na ufugaji na hivyo akawaahidi kuwa wakimchagua atashirikiana nao kutatua kero hiyo.

“Mimi nawaahidi kuwa nitakuwa daraja kati yenu na serikali, nitakuwa nawasikiliza na kuwasilisha mambo yenu serikalini, naamini kwamba Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ni msikivu sana na atasikiliza kilio chetu,” alisema Bahati.

Vilevile alisema katika Kata ya Madibira kuna matatizo mengi ambayo yanatakiwa kutatuliwa ikiwemo miundombinu ya barabara na madaraja ambayo yanatakiwa kujengwa ili kuwarahisishia shughuli zao za uzalishaji.

Alisema Wakala wa Barabara nchini (TANROAD) wamejenga daraja katika eneo hilo na limekamilika kwa muda mrefu lakini bado halijafunguliwa jambo ambalo linakwamisha shughuli zao.

Alisema ameshazungumza na Meneja wa wakala huo Mkoa wa Mbeya na amemhakikishia kuwa daraja hilo limeshakamilika lakini kilichobakia ni Shirika la Umeme nchini (TANESCO) kuondoa Nyaya za umeme ambazo zipo juu ya daraja hilo.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbarali, Mary Mbwilo alisema chama hicho kimejipanga kuhakikisha kinatetea jimbo hilo ili kiendelee kuwatumikia wananchi wa eneo hilo.

Alisema mgombea ambaye chama hicho kimemsimamisha ana ushawishi na hivyo wana uhakika atashinda na atafanya vizuri kazi ya kuwatumikia wananchi wa Wilaya ya Mbarali.

Alisema mgombea huyo ana uwezo mkubwa kwa maelezo kuwa hata wakati alipokuwa Mbunge wa Viti Maalumu kupitia Jumuiya ya Wazazi alikuwa anawatetea vizuri wananchi wa Mbarali hasa kuwasemea matatizo yao.

“Chama chetu kinakubalika sana katika maeneo karibia yote ya jimbo hili, lakini pia mgombea wetu anakubalika na makundi karibia yote ndani ya jimbo letu kwahiyo kazi yetu kama chama ni kumsaidia kuhakikisha anapata ushindi mkubwa,” alisema Mary.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Mwakibete jijini Mbeya, Lucas Mwampiki ambaye ni miongoni mwa watu wanaomsaidia Bahati kwenye kampeni aliwataka wananchi wa jimbo hilo kutodanganyika na maneno ya wapinzani.

Alisema baadhi ya watu wanaogombea kupitia vyama vya upinzani walikimbilia kwenye vyama hivyo baada ya kutoswa na CCM kutokana na tabia zao ambazo zilikuwa mbovu.

Uchaguzi mdogo unafanyika Mbarali kwa lengo la kuziba nafasi iliyoachwa na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Francis Mtega ambaye alifariki kwa ajali ya kugongwa na trekta wakati akiendesha pikipiki kwenda shambani.



Mgombea Ubunge wa Jimbo la Mbarali, mkoani Mbeya kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Bahati Ndingo, akihutubia mkutano wa kampeni katika Kata ya Madibira juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mbeya-WSSA yalaumiwa utoaji huduma

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa mitaa ya Ituha na Tonya katika Kata ya Ilomba jijini Mbeya, wameilalamikia Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), kushindwa kuwapatia huduma ya uhakika licha ya kununua vifaa na kujenga vituo vya pamoja.

Wananchi hao wanadai kuwa wanahangaika kwenda kutafuta huduma hiyo maeneo ya mbali hali ambayo inakwamisha baadhi ya shughuli zao za maendeleo.

Wakizungumza kwenye mkutano wa hadhara ulioshirikisha wananchi hao pamoja na watendaji wa mamlaka hiyo, walisema adha hiyo imesababisha baadhi yao kushindwa kuoga na kuhofia uwepo wa magonjwa ya mlipuko.

Mmoja wa wakazi hao, Grace Mwaipasi alisema tatizo la kukosekana kwa huduma ya maji katika maeneo yao ni kubwa hali inayosababisha kushindwa kufanya shughuli zao ikiwemo usafi kufua nguo kuoga pamoja na kupika.

“Tangu mamlaka ya maji walipofunga bomba za pamoja, tukaanza kutumia bomba binafsi maji yanatoka kwa shida, kwa wiki yanaweza kutoka mara mbili tu, serikali inasema inamtua mama ndoo kichwani, cha ajabu walioko vijijini wanapata huduma kuliko sisi,” alisema Grace.

Jackson Mbewa alisema pamoja na tatizo la kukosekana kwa huduma ya maji lakini wamekuwa wakipelekewa ankara kubwa ya maji kila mwezi na wakitakiwa kulia jambo ambalo linawapa wakati mgumu kulipia huduma ambayo hawaipati. Diwani wa Kata ya Ilomba, Hopes Chaula aliomba mamlaka kutumia mbinu mbadala kuwafikishia wananchi hao maji na ikiwezekana waifikishe kwa mgawo kama ambavyo taasisi zingine zinafanya likiwemo Shirika la Umeme nchini (TANESCO).

Alisema awali maeneo hayo yalikuwa na mradi wa maji ambao ulikuwa ukisimamiwa na wananchi na baadae usimamizi wake ukawa chini ya mamlaka ya maji, ambayo wananchi wanadai hawaridhishwi na utendaji wao wa kazi baada ya kukosekana kwa huduma ya maji.

Alidai kuwa mamlaka hiyo tangu ilipochukua mradi huo wa maji mwaka jana kutoka kwa wananchi haikuwahi kuweka miundombinu yake na badala yake imekuwa ikitumia miundombinu iliyowekwa na wananchi ambayo nayo haikidhi mahitaji.

Kaimu Mkurugenzi wa Mbeya-WSSA, Francis Mwaipashi alikiri uwepo wa tatizo la maji katika eneo hilo akisema linatokana na watu kuongezeka huku vyanzo vya maji vikiwa ni vilevile.

Mwaipashi alisema suluhisho la tatizo hilo litapatikana baada ya kuanza kwa mradi wa maji wa Mto Kiwira ambao alisema tayari umeanza utekelezaji wake.

## Kushusha ushuru chanzo h/shauri kukusanya mapato kiduchu

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Njombe mkoani Njombe imeshindwa kufikia asilimia 100 katika ukusanyaji mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ya kushushwa kwa ushuru wa mbao.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Valentino Hongoli, aliyasema hayo wakati akifungua mkutano wa kawaida wa baraza la madiwani.

“Asilimia 98 za ukusanyaji mapato ndizo zilizofikiwa na sababu kubwa ni kufanyika kwa marekebisho ya tozo za mbao kutoka shilingi 200 hadi shilingi 100 kwa ubao kwa maelekezo ya serikali kwa hiyo hali hiyo imesababisha kushuka kwa mapato tofauti na miaka mingine iliyopita,” alisema Hongoli.

Aliongeza: “Pamoja na changamoto hiyo lakini sababu nyingine ni baadhi ya watendaji kutowajibika ipasavyo, uzembe wa kukusanya maduhuri hayo ya serikali ni miongoni mwa kikwazo cha kukwamisha malengo yetu”.

Hongoli alisema serikali ilitoa pikipiki kwa maofisa watendaji wa kata, hivyo hataki kusikia sababu yoyote ya kutofuatiliwa kwa makusanyo kwenye vijiji.

Baadhi ya madiwani akiwemo, Vasco Mgunda na Isaya Myamba walisema uzembe unaofanywa na baadhi ya maofisa watendaji katika ukusanyaji mapato unasababisha wafanyabiashara wengi kutoroka na fedha jambo ambalo linapaswa kudhibitiwa.



## Makamu wa Rais ataja njia kuondoa tatizo la ajira kwa vijana

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema jamii inapaswa kuamini kwamba shughuli za kuendeleza sekta ya kilimo kibiashara kwa njia za kisasa ni fursa muhimu, itasaidia kupunguza tatizo la ajira kwa vijana wa Zanzibar.

Aliyasema hayo jana alipokutana na ujumbe wa Kampuni ya 'Quantaum' Infinite kutoka Dar es Salaam inayojishughulisha biashara katika vyombo vya habari pamoja na kuelimisha vijana katika kuzikabili changamoto za maisha.

Aliwataka vijana kujiongeza katika kuzitambua, kuziamini na hatimae kuzitumia fursa zitokanazo na sekta ya kilimo ambazo zikitumiwa vyema na vijana zinaweza kuwainua katika kulikabili ipasavyo tatizo la ajira nchini.

Makamu alisema kwamba kuna haja kubwa vijana kusaidiwa ili kuwa na mwamko mkubwa na kuzitumia ipasavyo fursa za aina mbalimbali zilizopo, zinazotokana na shughuli za kuendeleza kilimo.

Aidha, alisema hivi sasa Zanzibar kuna mahitaji makubwa ya bidhaa zitokanazo na sekta ya kilimo na iwapo itaendelezwa kwa juhudi na kwa njia bora upo uwezekano wa kusaidia vijana kuondokana na tatizo la ajira.

Alisema mahitaji yaliyopo ya sekta ya hoteli za utalii pekee kupitia bidhaa za kilimo ni makubwa na hadi sasa bidhaa nyingi zinazotumika katika hoteli zinapatikana kutoka nje ya Zanzibar.

Aidha, aliupongeza uongozi wa kampuni hiyo kwa kuwa wabunifu na kuweza kuanzisha na kuendeleza mashindano ya 'Ndondo Cup'.

Meneja msimamizi wa Kituo cha TV3 kinachomilikiwa na Kampuni ya Quantaum Infinite, Emmanuel Sikawa, alisema mashindao ya Ndondo Cup yamesaidia vijana wa Zanzibar kuwa na mwamko mkubwa.

Alisema jambo hilo limewapa hamasa ya kushiriki na kuunga mkono timu zao za mitaani na kuyafanya mashindano hayo kuwa yenye hamasa kubwa kwa vijana wote nchini.

Alisema mashindano hayo yaliyoanza miaka minane iliyopita yameanza kwa timu 30 na fainali itachezwa mwishoni mwa wiki kwa kuzishirikisha timu za Miembeni na Ubinaadamu Kazi kutoka Magomeni Zanzibar.

# 'Mradi wa 'heshimu bahari' kuimarisha viumbe baharini'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mkaazi wa Shirika la USAID Tanzania, Craig Hart amesema mradi wa heshimu bahari umelenga kuimarisha mazingira ya bahari na viumbe vyake katika maeneo ya hifadhi.

Amesema pia umelenga kukuza hifadhi ya bahari na kuongeza uzalishaji katika rasilimali za baharini na mazalia ya samaki.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wavuvi, wakulima wa mwani na kamati ya uvuvi na Wananchi wa Chwaka Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema mradi huo unaofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia shirika lake la misaada la USAID- Tanzania Bara ikiwemo Mkoa wa Tanga, Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es salaam na mikoa yote ya Unguja na Pemba ambao utagharimu Dola za Marekani milioni 25 hadi kukamilika kwake.

Hart alisema wanaunga mkono shughuli zinazofanywa na Rais Samia na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Mwinyi katika kuwaletea maendeleo wananchi.

Alisema anapenda kuonana na wanajamii ambapo USAID inafanya kazi nao kwa karibu kupitia mradi wa heshimu bahari, kusaidia sekta ya afya, elimu na shughuli zingine za kiuchumi.

**Mimi napenda sana samaki na hata mke wangu anapenda sana mwani, hivyo kama hatutoilinda bahari samaki watakosekana lakini pia mwani ni muhimu sana na una faida nyingi mwilini.**

Aidha, alisema ziara yake hiyo amejifunza mambo mengi ikiwemo changamoto za bahari na uvuvi haramu ambapo changamoto hiyo siyo kwa Tanzania pekee bali pia katika nchi mbalimbali zilizoendelea, hivyo ni vyema kudhibiti hali hiyo na kuwa na uvuvi endelevu ambao kila mmoja kufaidika nao.

Alisema amevutiwa na mandhari ya Zanzibar ambayo yamezungukwa na bahari, hivyo yanahitaji kulindwa ili wananchi kuendelea kufaidika na rasilimali zilizomo baharini ikiwemo uvuvi na ukulima wa mwani.

"Mimi napenda sana samaki na hata mke wangu anapenda sana mwani, hivyo kama hatutoilinda bahari samaki watakosekana lakini pia mwani ni muhimu sana na una faida nyingi mwilini," alisema.

Naye Mratibu wa mradi huo, Sadiki Laiser, alisema mradi pia umejikita katika kuimarisha sera zitakazosaidia serikali, sekta binafsi pamoja na jamii, kwenye kuimarisha, kuhifadhi, matumizi endelevu ya rasilimali za bahari.

Alisema mradi huo ni wa miaka mitano ambapo sasa unaelekea katika utekelezaji wake kwa awamu ya pili ili kuboresha ustawi wa kiikolojia na uzalishaji wa maeneo ya viumbe hai wa bahari Tanzania.

Mratibu huyo alieleza kuwa mradi huo pia unalenga kuwawezesha vijana na wanawake kiuchumi wakiwemo wakulima wa mwani, wafugaji wa majongoo bahari na wavuvi ili kuheshimu bahari na rasilimali hiyo kuwa endelevu.

Wakizungumza katika mkutano huo, wakulima wa mwani wa kijiji hicho, walisema wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa nyenzo zitakazowawezesha kufika katika mashamba yao ya mwani ambapo sasa wanalima katika kina kirefu cha maji ya bahari.

"Hatuna usafiri wa uhakika wa kutufikisha katika mashamba yetu ya bahari, tunaomba msaada kwa wavuvi watupakie katika boti zao za uvuvi na kutupelekea katika mashamba yetu. Wapo ambao baadhi yao wanakubali kutuchukua aidha kwa kulipia au kutupa msaada" alisema Khadija Juma Ame.

Pia, alisema wanahitaji nyenzo za kisasa kwa ajili ya kuendeleza kilimo hicho ambacho sasa kinakabiliwa na changamoto ya mabadiliko ya hali ya hewa yaliyotokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Hata hivyo, alisema bado bei ya mwani ni ndogo ambapo kilomoja huuzwa shilingi 1,000, hivyo wanahitaji kuongezewa bei kwa sababu kilimo cha mwani ni kigumu.

Khadija aliliomba Shirika na USAID kusadia masoko ya nje ya zao hilo la mwani ili kuongeza thamani ya mwani ambalo zao hilo ni mkombozi mkubwa wa wananchi hasa wanawake.



Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) Tanzania, Craig Hart (wa pili kulia), akizungumza na wavuvi, wakulima wa mwani na wananchi wa kijiji cha Chwaka, Mkoa wa Kusini Unguja jana, wakati alipotembelea kukagua uendeshaji wa mradi wa USAID Heshimu bahari. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kigogo CCM atoa somo kwa wazazi kuhusu elimu ya watoto

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Hemed Suleiman Abdulla, amewataka wazazi na walezi kuwasimamia watoto katika elimu ili taifa lipate wataalamu watakaosaidia kuleta mabadiliko hasa kipindi hiki cha sayansi na teknolojia.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wananchi wa Chonga na Ole Mkoa wa Kusini Pemba, alisema serikali imechukua jitihada katika kukuza sekta ya elimu ikiwemo ujenzi wa shule za ghorofa, uajiri wa walimu, ununuzi wa vifaa pamoja na maabara za kisasa ili vijana wawe na mazingira mazuri ya kujisomea.

Alisema ni wajibu wa wazazi kuthamini juhudi hizo kwa kuwahimiza watoto kusoma na kuwa na ushirikiano na walimu ili kufikia malengo ya kukuza elimu nchini.

Hemed alisema kuwa msimamo wa Serikali ni kuwaletea maendeleo wananchi wake na kuwawezesha kiuchumi, hivyo itahakikisha changamoto zilizobakia na zitakazojitokeza ikiwemo umeme, maji, barababara na kuwezeshwa kiuchumi zitatatuliwa kabla ya mwaka 2025.

Naye Mwakilishi wa Viti Maalum Mkoa Kusini Pemba, Shadya Muhamed, alisema Jumuiya ya Wanawake itawasimamia vijana wote ambao hawana kitambulisho cha mzanzibari kwa kuhakikisha wanasajiliwa na kupatiwa kitambulisho hicho.

Mkuu wa Wilaya ya Chakechake, Dk. Abdallah Rashid, alisema kuwa Serikali ya Zanzibar imefanya mabadiliko katika sekta mbalimbali katika wilaya hiyo ikiwemo sekta ya elimu, kwamba imejenga shule ya elimu mjumuisho eneo la Kijini ili watoto wenye mahitaji maalum wapate haki yao ya msingi ya elimu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

BWANA **HEKIMA LEONARD MASAKI** WA IRINGA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI **T321 AXW** .YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/417/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MOHAMMED ENTERPRISES TANZANIA LTD** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya ***BAJAJ BOXER*** yenye usajili namba **MC 443 CH**F na CHASSIS NAMBA: **MD2A21BY2KWD85968.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **SOG/RB/3945/2023**

## KUPOTELEWA NA VYETI



Ndugu **GODFREY KISILI BWANA** anatangaza kupotelewa na cheti cha shule ya sekondari Paroma ya mkoani Mara chenye namba **S4576-0073** cha mwaka 2012 na vya Chuo cha Uhasibu Tanzania chenye namba **MZA/BCPLM/13/14971** cha mwaka 2014 na **MZA/DPLM-E/15/32176** cha mwaka 2017. Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **PHQ/DOD/CHA/1230/2023.** Kwa yeyote atakayeviona atoe taarifa polisi au apige simu namba 0758401160.

## KUPOTEA KWA CHETI



**FRANCIS GASPAR CHOPA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.5111-0006** kilichotolewa na Baraza La Mitihani La Taifa kupitia MURIET SPRING SECONDARY SCHOOL mwaka 2018. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: ARU/MUR **RB 216269/2023**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 101 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE MTM 93211SGT MARTHA MBOKIGWE SWILLA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION PROBATE BY DEBORA MBOKIGWE SWILLA**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 of PROBATE RULES GN 369 OF1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 20 day of 09...............2023
**Dated at Dodoma this 14day of 08..................................2023**

Date at Dodoma this ......14..........Day of ....08..........................2023.


PETITIONER

Presented for filing this.......30......................day of...08....2023

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE I/c
DODOMA DISTRICT

## SPECIAL POWER OF ATTORNEY

I, JOE SANDRESS KONDOWE of phone number 0672 951093 Dar es Salaam, [herein referred to as the `DONOR' ]DO HEREBY APPOINT MIKIDADI JUMA ABDALLAH of phone number 0678411495 Dar es Salaam [herein referred to as the "DONEE" ] who is the resident of MJIMWEMA KIGAMBONI , DAR ES SALAAM, to be a lawful Attorney of the Donor and on his behalf process and sign DOCUMENTS and any Documents incidental thereto and REPRESENT the Donor of any matter in Court concerning the case number 67 of 2023 between HAMZA JUMA RASHIDI versus JOE S. KONDOWE AT DISTRICT Land and Housing Tribunal at Kigamboni Mvumoni Geita.
Also to take care of all property including business premises local at Mjimwema Kigamboni
This Power of Attorney may not be assigned or transferred to any other person
I HEREBY Declare that the particular power enumerated above shall be given the widest interpretation and shall not be construed as setting limits on the power construed as setting limit on the power conferred on my Attorney.
IN WITNESS WHEREOF I have hereunto set my hand and Seal on this 16th Day of August.2023



**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 102 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ANNASTAZIA AMANDUSI FIRIMINI**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR APPOINTMENT OF ADMINISTRATIX OF A SMALL ESTATE BY RAHEL ANOLD MMARI**

**FORM 58**

**APPLICATION FOR APPOINTMENT OF ADMINISTRATIX OF SMALL ESTATE**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 20 day of 09...............2023
Dated at Dodoma this 30 day of 08...........................2023

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE I/c
DODOMA DISTRICT

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**LA WILAYA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**
**MAOMBI NA 154 YA MWAKA 2020**
**SHEMA MALEKELA......... MDAI**
**VERSUS**
**ELIAS JOHN MDAO............MDAIWA 1**
**MATATA MJITI MPINNA...............MDAIWA 2**

**KWA: MATATA MJITI MPINNA**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Dodoma wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 04.09.2023 saa 3.00 asubuhi Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
ANGALIZO: - Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza Likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 04 ya Mwezi wa AGOSTI, 2023.

3.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA
NYUMBA LA WILAYA YA
DODOMA
TANZANIA


***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701***

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 0677020701**

**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Rais Gabon Ali Bongo apinduliwa, kizuizini

**Libreville, GABON**

VIONGOZI wa kijeshi nchini Gabon wametangaza kuchukuwa madaraka, siku chache baada ya taifa hilo, kufanya uchaguzi na kumrejesha madarakani, Rais Ali Bongo Ondimba, kwa muhula wa tatu.

Baadhi ya mitaa kwenye mji mkuu Libreville, wananchi walionekana jana wakishangilia kutokana na mabadiliko hayo, huku jeshi likieleza kumuweka kizuizini Ali Bongo.

Muhula huu, ungeweka historia kwenye familia yake ya Bongo, ambayo imetawala kwa zaidi ya miaka 55, baada ya rais huyo, kutwaa madaraka mwaka 2009 kutoka kwa baba yake Omar Bongo.

Omar Bongo, alitawala kuanzia mwaka 1967 hadi kifo chake. Gabon ina watu karibu milioni 2.3, wengi wao wakiishi kwenye umaskini.

Maofisa wa jeshi walionekana kwenye televisheni ya taifa nchini Gabon, wakisema wamechukua mamlaka.

Chanzo cha mapinduzi hayo kinatajwa ni uchaguzi wa wikiendi iliyopita, Agosti 26, mwaka huu, ulioibua ukosoaji, baada ya serikali kuzuia upatikanaji wa huduma za mtandao kura zikihesabiwa.

Amri ya kutotoka nje ilitangazwa kuanzia saa moja jioni, juzi hadi saa 12 asubuhi, jana. Vituo kadhaa vya kimataifa kama Redio France, vilipigwa marufuku kutangaza.

Viongozi hao wa kijeshi kupitia televisheni, walisema wamefuta matokeo ya uchaguzi wa Jumamosi, wiki iliyopita yaliyompa ushindi, Rais Ali Bongo.

Mapinduzi hayo ni chini ya mwezi mmoja baada ya walinzi wa Rais wa Niger, kumpindua Rais aliyechaguliwa kidemokrasia, Mohamed Bazoum.

Kadhalika, viongozi wa kijeshi nchini Mali na Burkina Faso, walichukua madaraka na kusababisha hali ya wasiwasi na demokrasia katika ukanda huo wa Magharibi



**UCHAGUZI WIKI JANA**

Uchaguzi mkuu uliofanyika Jumamosi iliyopita, ulikumbwa na ukosefu wa waangalizi wa kimataifa na maombi ya waandishi wa habari wa kigeni kupewa vibali vya kuripoti kukataliwa.

Tume ya uchaguzi ilisema, Ali Bongo alishinda chini ya theluthi mbili tu ya kura katika uchaguzi ambao upinzani ulidai kuwa ulikuwa wa udanganyifu.

Wanajeshi 12 walionekana kwenye televisheni wakitangaza kuwa wanafuta matokeo ya uchaguzi na kuvunja taasisi zote za jamhuri.

Mmoja wa wanajeshi hao kwenye chaneli ya televisheni ya Gabon 24: "Tumeamua kulinda amani kwa kukomesha utawala uliopo." Hii, aliongeza, ilikuwa chini ya utawala usiowajibika, usiotabirika na kusababisha kuzorota kwa uwiano wa kijamii, ambao unahatarisha nchi katika machafuko".

Mawaziri wa Ulinzi wa Umoja wa Ulaya (EU), wanatarajiwa kuijadili Gabon, Mkuu wa Sera za Kigeni wa Baraza hilo, Josep Borrell, alisema.

"Iwapo hili litathibitishwa, ni mapinduzi mengine ya kijeshi ambayo yanaongeza ukosefu wa utulivu katika eneo zima."

"Eneo zima, kuanzia Jamhuri ya Afrika ya Kati, kisha Mali, kisha Burkina Faso, sasa Niger, Gabon, hali ni ngumu sana... inabidi mawaziri watafakari kwa kina nini kinaendelea huko, jinsi tunavyoweza kuboresha sera yetu kwa heshima na nchi hizi," alisema.

**JARIBIO 2019**

Hali ya kisiasa nchini iliwahi kutikiswa pia mwaka 2019 baada ya jeshi kufanya jaribio la kumpindua rais huyo huyo.

'Gabon ni shuwari na salama," Msemaji wa Serikali Guy-Bertrand Mapangou alisema, wakati huo, baada ya wanajeshi waaminifu kwa serikali ya Rais Ali Bongo, kufanikiwa kuzima jaribio la mapinduzi ya serikali nchini humo.

Tayari wanajeshi wote watano waliohusika katika mapinduzi hayo, walikamatwa na mamlaka.

**BONGO NI NANI**

Ali Bongo Ondimba, alizaliwa Februari 9, mwaka 1959 mjini Brazzaville na alifahamika kama mwana wa Alain Bernard Bongo (ambaye baadaye alifahamika kama Omar Bongo Ondimba) na Josephin Kama (baadaye Patience Dabany).

Mjadala upo kwamba, Je, Ali Bongo ni mwana wa Omar Bongo ikizingatiwa, mama yake alikuwa mjamzito miezi 18 kabla ya kuolewa.

Madai hayo, Ali Bongo amekuwa akiyapinga. Aidha, wakati wa kuzaliwa kwake mama yake alikuwa ana miaka 15.

Ali Bongo, alipohitimu uanasheria, alijitosa katika siasa za Gabon na alijiunga na chama PDG mwaka 1981 na muda mfupi baadae, aliteuliwa katika Kamati Kuu ya chama Machi, mwaka 1983.

Baadae aliteuliwa kumwakilisha baba yake katika chama hicho, nafasi ambayo ilimwezesha kujiunga na asasi kuu ya uongozi wa chama katika uamuzi ambao ulifikiwa katika kongamano maalum ya PDG mwaka 1986.

Ali Bongo, ni mwana wa kiume wa Rais Omar Bongo, ambaye aliongoza Gabon kimila kutoka mwaka 1967 hadi alipofariki dunia mwaka 2009.

**BBC/DW**

## Harusi ya mashoga yatibuliwa

**Lagos, NIGERIA**

WATU 200 wamekamatwa katika hafla ya harusi ya mashoga, iliyofanyika katika hoteli moja karibu na mji wa pwani wa Warri, jimbo la Delta, kusini mwa nchi hiyo.

Msemaji wa Polisi katika jimbo hilo, Bright Edafe alisema wengi wa wanaume waliohudhuria harusi hiyo walivaa nguo za kike.

Wanaume wawili waliovalia nguo za bwana na bibi harusi pia wamekamatwa.

Edafe, aliongeza kwamba, waliokamatwa watafunguliwa mashtaka, pindi uchunguzi dhidi yao utakapokamilika.

Nigeria, nchi yenye watu wengi zaidi barani Afrika ikiwa na karibu watu milioni 220 ilipitisha sheria mwaka 2014 kupiga marufuku mapenzi ya jinsia moja.

**DW**

## Usiri watawala maziko ya Prigozhin

**St. Petersburg, RUSSIA**

MKUU wa Kikundi cha Wagner, Yevgeny Prigozhin, amezikwa katika ibada ya maziko binafsi huko St. Petersburg, kulingana na ofisi yake ya waandishi wa habari.

Maziko hayo yalifanyika kwa siri na waliotaka kumuaga walitakiwa kutembelea makaburi ya Porokhovskoye.

Awali, maofisa wa Russia, walithibitisha kifo cha mkuu wa kundi hilo, baada ya kufanya uchambuzi wa vinasaba wa miili 10 kwenye ndege iliyoanguka wiki iliyopita, Agosti 24, mwaka huu.

Ajali hiyo ilitokea karibu na mji wa Moscow, huku Kremlin ikikanusha uvumi ulioibuka kuwa ilisababisha ajali hiyo.

Tovuti ya Kirusi, pia ilisema kwamba, Prigozhin alizikwa karibu na kaburi la baba yake na bendera nyeusi, njano na nyekundu ya Wagner, ikiwekwa.

Shirika la habari la Fontanka la Saint Petersburg, liliripoti kwamba vizuizi vya chuma viliwekwa kwenye lango, inaaminika kuwa viongozi wanajiandaa kufanya hija kubwa kwenye kaburi la Prigozhin.

Lakini idadi kadhaa ya waangalizi wa Russia, ndani na nje ya nchi, wamemuelezea Prigozhin (62), kama mtu aliyekufa akitembea tangu uasi wake aliouongoza dhidi ya serikali ya Rais Vladimr Putin, Juni mwaka huu.

**BBC**

# INONGA, KRAMO WAKO FITI WAANZA MAZOEZI SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imetangaza rasmi kuwa wachezaji wake wawili Aubin Kramo na Henock Inonga waliokuwa majeruhi, wameanza mazoezi kwa ajili ya maandalizi ya mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya raundi ya kwanza dhidi ya Power Dynamos ya Zambia.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema wachezaji hao walianza mazoezi juzi kwenye Uwanja wa Mo Arena, Bunju, baada ya kuwa nje kwa zaidi ya wiki mbili wakiwa majeruhi.

"Kikosi kilianza mazoezi Jumanne iliyopita, wachezaji wetu wote wamerejea kambini na bahati nzuri hakuna mchezaji ambaye alisafiri nje ya nchi na taarifa njema ambayo wanachama na mashabiki wa Simba wanapaswa kuifurahia ni kwamba Aubin Kramo ameanza mazoezi, kumbuka alipewa wiki moja ya mapumziko, amefanya mazoezi jana jioni (juzi) akiwa yupo fiti kabisa, vile vile beki wetu wa kati Henock Inonga naye amerejea, yeye alipewa muda mrefu kidogo wa kupumzika ila kwa sasa yuko timamu na amefanya mazoezi na wenzake, kikubwa tuko tayari kuelekea kwenye mchezo wetu wa raundi ya kwanza Ligi ya Mabingwa dhidi ya Power Dynamos," alisema Ahmed.

Inonga aliumia katika mechi ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii dhidi ya Singida Fountain Gate Agosti 10 na Kramo aliumia mazoezini kabla ya michezo ya Ngao ya Jamii.

Klabu hiyo pia imesema itacheza mechi moja au zaidi za kirafiki kwa ajili ya kuwaweka fiti wachezaji wake kutokana na kukaa muda mrefu bila kucheza.

"Kwa mujibu wa kocha wetu ni lazima tupate mechi za kirafiki moja au zaidi, mara ya mwisho tulicheza dhidi ya Dodoma Jiji, tumekaa muda kidogo na kuna wiki nyingine za kukaa bila michezo kwa hiyo lazima tucheze mechi za kirafiki ili kunyanyua utimamu wa mwili na pumzi za wachezaji," alisema Ahmed.

Aidha, alisema kuwa klabu hiyo imepata barua rasmi kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) kuwa mechi yao itachezwa Jumamosi ya Septemba 16 Uwanja wa Levy Mwanawasa Ndola, Zambia.

"Mipango inafanywa ili wanachama na mashabiki wetu nao wasafiri kwa basi na wengine kwa treni ya TAZARA ili kwenda kuwapa nguvu wachezaji wetu," alisema Meneja Habari huyo.

# Wavu taifa kukiwasha Misri

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya mpira wa wavu ikiwa na wachezaji 12 inatarajiwa kuondoka nchini kesho kwenda Misri kushiriki mashindano ya Afrika kwa wanawaume yaliyopangwa kuanza Septemba 3-14.

Akizungumza na gazeti hili jana, jijini Dar es Salaam Kocha Mkuu wa timu hiyo, Alfref Serengia, alisema maandalizi ya safari hiyo yamekamilika na wamefanya maandalizi ya kutosha kwa ajili ya michuano hiyo.

"Maandalizi yanaendelea vyema na keshokutwa ( kesho ) tunatarajia kuanza safari yetu kuelekea nchini Misri, tunaomba watanzania watuombee ili tukaiwakilishe vizuri nchi yetu na kupeperusha vyema bendera ya Taifa letu," alisema Serengia.

Aidha, alisema awali walitarajia waondoke na wachezaji 14 lakini kutokana na uhaba wa fedha wamelazimika kupunguza wachezaji wawili na kuondoka na wachezaji hao 12.

Kocha huyo aliishukuru Serikali kutokana na juhudi walizozifanya kufanikisha timu hiyo inapata nafasi ya kwenda kushiriki michuano hiyo.

Wakati huo huo, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mpira wa Wavu Tanzania( TAVA), Laurence Safari, amewataka wachezaji hao wa timu ya taifa kuhakikisha wanaenda kupambana na kurudi na ushindi nyumbani.

Timu hiyo watafanya mazoezi yao ya mwisho leo kwenye uwanja wa Gwambina (zamani TCC Chang'ombe) kabla ya kesho kuanza safari.

# Simon Msuva akomalia soka la kimataifa

**Rakim Jumanne (SAUT) na Florah Francis (SJMC)**

NYOTA wa timu ya taifa 'Taifa Stars' Simon Msuva, ameweka wazi kuwa kwa sasa hana mpango wa kurudi kucheza soka nchini na ndio sababu ya kujiunga na klabu ya JS Kabylie ya Algeria.

Msuva ambaye hivi karibuni alikuwa akihusishwa kutakiwa na klabu za Simba na Yanga, juzi alitangazwa kujiunga na timu hiyo inayoshiriki ligi kuu ya Algeria.

Msuva alikiri kuwa ni kweli alikuwa akitakiwa na vigogo hao wa soka nchini lakini kwa sababu bado ana shauku la kuendelea kucheza nje ya nchi aliamua kujiunga na JS Kabylie.

"Najiona bado nina nafasi ya kuendelea kucheza soka la kulipwa nje ya nchi, ndio maana ilikuwa ngumu kwangu kukubaliana na ofa za Simba na Yanga ambazo zilikuwa nzuri tu, wakati ukifika nitarudi na kumalizia mpira wangu nyumbani hilo lipo wazi," alisema nyota huyo wa zamani wa klabu za Difaa el Jadida na Wydad Casablanca za Morocco.

Msuva alisema muda ukifika atarejea nchini kumalizia soka lake lakini kwa sasa bado anajihisi mwenye nguvu kucheza soka la kimataifa na kuendelea kuitumikia timu ya taifa.

"Nimejiunga na JS Kabylie kwa sababu ya uwezo wangu, bado natamani kuendele kucheza soka nje ya nchi na pia kuendelea kutumika kwenye timu yangu ya taifa.., soka ni kazi yangu na naifanya kwa umakini mkubwa," aliongeza kusema Msuva.

Kabla ya kwenda kucheza soka nje ya nchi, Msuva aliwahi kuzichezea klabu za AZAM FC na Yanga iliyompa umaarufu mkubwa na kupata nafasi ya kusajiliwa Difaa El Jadida ya Morocco mwaka 2017 akitoka Jangwani.



Watoto wakicheza mpira wa Magongo katika viwanja vya kituo cha kukuza vipaji cha Jakaya Kikwete, jijini Dar es Salaam kama walivyokutwa na mpiga picha jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mashindano ngumi taifa kuanza leo

**Na Abdallah Mataka**

MASHINDANO ya ngumi ya klabu bingwa taifa kwa mwaka huu yanaanza kutimua vumbi leo kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga huku zaidi ya mabondia 120 wakishiriki.

Mashindano hayo ambayo yanasimamiwa na Shirikisho la ngumi za ridhaa nchini (BFT) kwa kushirikiana na wenyeji Chama cha Ngumi Mkoa wa Tanga yatakuwa sehemu ya kupata wachezaji watakaoongezwa kwenye Timu ya Taifa ya ngumi inayojiandaa kushiriki mashindano ya kufuzu Olimpiki kwa Bara la Afrika yatakayofanyika jijini Dakar, Senegal September mwaka huu.

Akizungumza na Gazeti hili, Katibu Mkuu wa BFT, Makore Mashaga, alisema maandalizi yote kuelekea kwenye mashindano hayo yamekamilika na leo mabondia wanaanza kupanda ulingoni.

"Tayari tumeshafanya zoezi la uhakiki wa taarifa za washiriki (sports entry Chek) pamoja na vipimo vya afya na jumla ya washiriki 122 wamefanikiwa kufaulu vipimo hivyo" alisema Mashaga.

Mashaga pia alisema kuwa wametoa tahadhari ya matumizi ya dawa za kusisimua misuli michezo kwa mabondia wote na kusema kuwa hawatamvumilia bondia yoyote atakayepatikana na akitumia dawa hizo.

"Nitoe wito kwa mabondia matumizi ya dawa hizo hayatakubalika na bondia yeyote atakayebainika hatua kali zitachukuliwa dhidi yake ikiwemo kuondolewa kwenye mashindano, tumejipanga vizuri kudhibiti hilo tupo sambamba na timu ya madaktari ambao tutashirikiana pamoja katika suala hilo"alisema Mashaga

Alisema mabondia wengine watakaoonesha vipaji zaidi wataongezwa katika tmu ya Taifa kwa ajili ya mashindano mengine mbalimbali ya kimataifa yakiwemo mashindano mapya ya Afrika Mandela Cup yatakayofanyika Oktoba mwaka huu nchini Afrika Kusini.

## ZISIKUPITE

### TONEY ANUKIA CHELSEA

CHELSEA inaweza kuwasilisha ofa ya kumnunua mshambuliaji wa Brentford na England anayekadiriwa kuwa na thamani ya pauni milioni 80, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 27 kabla ya dirisha la usajili kufungwa kesho Ijumaa. **(Independent)**

### DIER KUTIMKIA BAYERN

KLABU ya Tottenham Hotspur imewapa Bayern Munich nafasi ya kumsajili beki wa England, Eric Dier mwenye umri wa miaka 29. **(Sky Sports)**

### TAGLIAFICO ATAKIWA MAN

MANCHESTER United imewasiliana na Lyon kuhusu uhamisho wa mkopo kwa beki wao wa kushoto raia wa Argentina, Nicolas Tagliafico mwenye umri wa miaka 30. **(Le Parisien)**

### MASON AWANIWA BESIKTAS

KLABU ya Besiktas inatazamiwa kumpa mshambuliaji wa Manchester United, Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 21 ofa ya kurejea kwenye soka baada ya kutangazwa kuwa ataondoka Old Trafford. **(i sport)**

### CACURRELLA ATAJWA MAN

MANCHESTER United pia imewasilisha pendekezo la kumsajili beki wa kushoto wa Hispania, Marc Cucurella mwenye umri wa miaka 25 kwa mkopo kutoka Chelsea. **(Mail)**

### GALLAGHER NA BAYERN

CHELSEA imepokea ripoti ofa kutoka kwa Bayern Munich kuhusu kiungo wa kati wa England, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 23, huku mlinzi wa England, chini ya umri wa miaka 21, Trevoh Chalobah mwenye miaka 24, pia akiwa tayari kuhamia kwa mabingwa hao wa Bundesliga. **(talkSPORT)**

### JOAO KURUDI CHELSEA

KLABU ya inafikiria kuchukua hatua ya kumrejesha mshambuliaji wa Atletico Madrid na Ureno, Joao Felix baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 kucheza kwa mkopo kule Stamford Bridge msimu uliopita. **(90 min)**

### LENGLET ATAKIWA VILLA

KLABU ya Aston Villa ipo kwenye mazungumzo na Barcelona kuhusu mpango wa kumnunua beki wa Ufaransa, Clement Lenglet mwenye umri wa miaka 28. **(Fabrizio Romano)**

### IWOBI ATAKIWA FULHAM

FULHAM ipo kwenye mazungumzo ya kiwango cha juu na Everton ili kumsajili kiungo wao wa kati wa Nigeria, Alex Iwobi mwenye umri wa miaka 27. **(talkSPORT)**

### LINGARD KURUDI WEST HAM

KUNA uwezekano mkubwa kwamba West Ham watampa mchezaji huru na kiungo wa zamani wa England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 30, mkataba wa muda mfupi. **(Standard)**

### GONZALEZ AWINDWA WOLVES

KLABU ya Wolves inapanga kumnunua mshambuliaji wa Club Libertad wa Paraguay, Enso Gonzalez mwenye umri wa miaka 18. **(Football Insider)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MAN UNITED WAJITOSA KUMSAJILI CUCURELLA

Inataka kumsajili Muhispania huyo ili kuziba pengo la Luke Shaw ambaye...

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United inajiandaa kumsajili mlinzi wa kushoto wa Chelsea, Marc Cucurella, kwa mujibu wa ESPN.

Man United ina nia ya kumsajili raia huyo wa Hispania kwa mkopo ili kuziba pengo la walinzi, Luke Shaw na Tyrell Malacia, ambao wote wanaweza kuwa nje ya uwanja hadi Novemba kutokana na majeraha.

Ofa iliyotolewa kwa Chelsea, kulingana na vyanzo, inajumuisha ada ndogo ya mkopo na malipo ya mshahara wa Cucurella.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 ana ziada ya mahitaji kutoka Stamford Bridge mwaka mmoja tu baada ya uhamisho wake wa pauni milioni 55 kutoka Brighton.

Cucurella bado hajacheza chini ya kocha mpya Mauricio Pochettino msimu huu na Chelsea wameweka wazi wanaweza kumruhusu kuondoka majira haya ya joto.

United wako sokoni kutafuta beki wa kushoto baada ya kuwapoteza Shaw na Malacia, na kumruhusu chaguo la tatu Brandon Williams kujiunga na Ipswich Town kwa mkopo.

Diogo Dalot alijaza nafasi ya beki wa kushoto kwa ushindi wa 3-2 dhidi ya Nottingham Forest Jumamosi na Alvaro Fernandez mwenye umri wa miaka 20, aliwekwa benchi.

Cucurella ni mojawapo ya chaguo za muda mfupi zilizotambuliwa na United, pamoja na Marcos Alonso, Nicolas Tagliafico na Sergio Reguilon.

Vizuizi vya Haki ya Kifedha vinamaanisha kuwa mpango wowote utalazimika kuwa wa bei ya chini iwezekanavyo.

Kocha Erik ten Hag tayari ametumia zaidi ya pauni milioni 160 msimu huu wa joto kuwasajili Andre Onana, Mason Mount na Rasmus Hojlund.

Pamoja na mabeki wa kushoto, United pia wanaangalia viungo katika siku za mwisho za dirisha la uhamisho, ingawa dili likitokea kuna uwezekano wa kuwa kwa mkopo.

Donny van de Beek na Eric Bailly bado wako tayari kwa uhamisho.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,148,6

MECHI KALI
SINGIDA BS FC
VERSUS
KITAYOSCE FC
1 | 1.44
X | 4.05
2 | 6.71

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Boniface Lwoga - 0654 330 XXX
2. Iman Kabonge - 0654 586 XXX
3. Lambat Lutalemwa - 0679 601 XXX
4. Christina Kiwele - 0679 660 XXX
5. Chrizostom Kalunde - 0679 800 XXX
6. Habiba Kipara - 0712 370 XXX
7. Salehe Chambasi - 0712 457 XXX
8. Vicent Sumuni - 0715 283 XXX
9. John John - 0718 685 XXX
10. Hamis Mawenje - 0719 195 XXX
20,000/= KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# HAZARD AZIKATAA TIMU, APANGA KUSTAAFU



**MADRID, Hispania**

KIUNGO mshambuliaji wa Ubelgiji, Eden Hazard amepanga kustaafu soka akiwa na umri wa miaka 32, huku ikidaiwa amegomea ofa kibao za kwenda kucheza soka nchini Saudi Arabia na Marekani.

Mkali huyo aliyeitumikia timu ya taifa ya Ubelgiji mara 126 aliripotiwa pia kuzivutia timu za Vancouver Whitecaps, Nice, Marseille na timu yake ya zamani Lille, zote zikitajwa kuhitaji huduma yake. Kwa mujibu wa ESPN Hazard amepanga kuachana na ofa hizo na dhamira yake kuu ni kuachana kabisa na kucheza soka, huku jambo hilo likisubiri tu kutangazwa.

Hazard ameshindwa kucheza kwa ubora kama ule alionesha alipokuwa akiitumikia Chelsea kwa miaka saba baada ya kujiunga na Real Madrid kwa ada ya pauni milioni 115 mwaka 2019.

Ukiweka kando janga la majeruhi ambayo yamekuwa yakimwandama sana, kulikuwa na shida nyingine kwenye ufiti wa mchezaji huyo ikiwamo kuongezeka uzito.

Hazard alistaafu soka la kimataifa baada ya Ubelgiji kutolewa mapema kwenye fainali za kombe la Dunia 2022 zilizofanyika nchini Qatar.

Akiwa hana timu yoyote tangu mkataba wake kule Real Madrid kumalizika Juni mwaka huu, imeelezwa mchezaji huyo anafikiria zaidi kustaafu kuliko kutafuta timu nyingine ya kwenda kuendeleza soka lake.

# Joao kumbadili Salah Liverpool

**LIVERPOOL, England**

MSHAMBULIAJI wa Atletico Madrid, Joao Felix anaangaliwa na mabosi wa Liverpool kama mbadala wa Mohamed Salah ambaye anahusishwa kwenye mpango wa kutaka kutimkia Saudi Arabia ambako Al litihad inamwania kumsajili.

Felix mwenye umri wa miaka 23, amekuwa kwenye sintofahamu katika dirisha hili kwani hayupo kwenye mipango ya kocha wa Atletico, Diego Simeone na timu ambazo zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili hadi sasa hazijawasilisha ofa rasmi.

Ingawa bado hakuna mazungumzo yoyote yaliyoanza hadi sasa, lakini ndani ya muda mfupi tayari Liverpool imeanza kujiandaa na ilikuwa na kikao na Salah Jumatatu ambacho kilikuwa kinajadili hatma ya kila kitu.

Mabosi wa Liverpool wanamuangalia Felix kwa sababu ndiye anayeonekana kuwa anaweza kupatikana kirahisi kwani vigogo wa Atletico wameweka wazi kwamba wapo tayari kumuuza.



Hata hivyo, mbali na Felix, Liverpool inapambana kupata huduma za Ryan Gravenberch kutoka Bayern Munich na Cheick Doucoure kutoka Crystal Palace katika siku chache za dirisha hili zilizobakia.

43,241/-

# PLUIJM AANIKA SABABU ILIYOMKIMBIZA SINGIDA

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Singida Fountain Gate FC, Hans van der Pluijm, amesema kitendo cha kuingiliwa katika majukumu yake, ndio chanzo cha yeye kuamua kuacha kuendelea kuifundisha timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, imefahamika.

Hata hivyo, uongozi wa klabu hiyo umetoa taarifa ya kuachana na Mholanzi huyo ambaye alipewa mkataba mpya baada ya ule wa awali kumalizika ilipofika Juni 30, mwaka huu.

Ofisa Habari wa timu hiyo, Hussein Masanza, alisema pande zote mbili zimefikia makubaliano na sasa timu hiyo itakuwa chini ya Kocha Msaidizi, Mathias Lule.

Kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana jijini zinasema Pluijm amefikia kufanya uamuzi wa kujiuzulu kwa sababu ya kutokubali kuingiliwa majukumu yake ikiwamo upangaji wa kikosi. Chanzo hicho kiliendelea kusema kitendo cha kukosa uhuru wa kufanya kazi ikiwapo kuingiliwa kupanga kikosi katika mchezo wa marudiano ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika walipocheza dhidi ya JKU.

"Huu mchezo tulipoteza kwa mabao 2-0, ila matokeo ya mechi ya kwanza yalitusaidia kwa sababu tulishinda magoli 3-1, matokeo hayo yametufanya tuendelee kusonga mbele. Sababu ya kujiuzulu ni bosi mmoja wa juu kumwingilia majukumu yake katika kupanga kikosi," kilisema chanzo chetu.

Pluijm aliyeiwezesha timu hiyo kumaliza nafasi ya nne msimu uliopita na kupata tiketi ya kushiriki michuano hiyo ya CAF na kufanikiwa kufuzu hatua ya kwanza.

Singida Fountain Gate imekuwa timu ya kwanza kuachana na kocha wake tangu kuanza kwa msimu wa Ligi Kuu Bara hapo Agosti 15, mwaka huu.

# Makali ya Yanga ni kipindi cha pili

INATOKA UK. 24

ua ya awali ambapo ilicheza dhidi ya ASAS Djibouti FC, imefunga mabao manne kati ya saba katika kipindi cha pili.

Agosti 20, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex iliichapa ASAS mabao 2-0, moja likifungwa kipindi cha kwanza na Aziz Ki dakika ya 22 na Musonda kipindi cha pili dakika ya 53.

Mechi ya marudiano Agosti 26, mwaka huu iliposhinda mabao 5-1, magoli mawili yalifungwa kipindi cha kwanza na matatu yalifungwa kipindi cha pili kupitia kwa Pacome dakika ya 51, Mzize (68) na Nzengeli (90).

Yanga sasa ndio vinara katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza ikiwa na pointi sita sawa na Azam FC na Simba, lakini yenyewe ikiwa na idadi kubwa ya mabao ya kufunga.

Kikosi hicho cha Jangwani kimefunga mabao 10 katika mechi mbili, Azam inafuata katika msimamo ikiwa na magoli saba na Simba iko katika nafasi ya tatu.

Akizungumza na Nipashe baada ya kufunga mabao 10 katika mechi mbili za Ligi Kuu Tanzania Bara alizocheza, Gamondi aliweka wazi kila mchezaji wa Yanga anaweza kufunga mabao ambayo yataisaidia timu hiyo kufikia malengo.

Gamondi alisema anahitaji kuona kila mchezaji ndani ya timu hiyo anafunga pale nafasi ya kufanya hivyo inapopatikana na hiyo itasaidia kuwaimarisha kufanya vizuri katika kila mechi.

Kocha huyo alisema ili kuachana na hali ya kutegemea washambuliaji peke yake, amebadilisha mfumo alioukuta na anataka kuona kila mchezaji aliyekuwa kwenye nafasi ya kufunga anatumia vyema nafasi wanazotengeneza.

"Hatuwezi kuwategemea washambuliaji pekee kutufungia mabao, nimebadili mfumo na kuwataka wachezaji wangu kila aliyekuwa katika nafasi basi anauwezo wa kufunga.

Ukiangalia katika mchezo wa leo (juzi), JKT Tanzania kipindi cha kwanza walicheza kwa kuzuia lakini tulipofanikiwa kupata bao la kwanza kupitia kwa Aziz Ki tulitengeneza hali ya kujiamini na kupambana kuelekea katika kipindi cha pili ambacho tulifanikiwa kufunga magoli zaidi," alisema Gamondi.



Aliongeza mchezo ulikuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu wapinzani wao (JKT Tanzania) walivyokuwa wanacheza kabla ya kuanza kupata bao la kwanza na baada ya bao la kwanza nyota wake walijiamini na kutengeneza nafasi na kufanikisha kile alichokifanya mazoezini.

Kiungo wa Yanga, Khalid Aucho, alisema siri kubwa ya kufanikiwa kufunga mabao matano katika kila mechi ni kufuata maelekezo ya benchi la ufundi na wachezaji kuonyesha kiwango kizuri kwa kutumia nafasi wanazotengeneza.

"Ni kweli tumefanikiwa kufunga mabao 10 katika mechi mbili za ligi, magoli matano katika mechi ya marudiano ya kimataifa, haya ni mafanikio ya kocha kuhitaji kuona kila mchezaji anacheza mpira na kufuata maelekezo na kutumia vizuri kila nafasi tunazotengeneza, na yoyote aliyekuwa kwenye nafasi anafunga," alisema Aucho.

## Simba yajipanga, Bocco, Mkude warejeshwa Stars

INATOKA UK. 24

mos ni timu nzuri, nadhani kila mmoja anakumbuka walivyocheza na sisi hapa kwenye Simba Day, lakini Simba ni klabu kubwa Afrika, tunajipanga kuanza na hesabu za kushinda ugenini ili tumalizie mchezo hapa nyumbani," alisema Robertinho.

Wakati huo huo, nahodha wa Simba, John Bocco, amerejeshwa katika kikosi cha Stars kitakachoingia kambini kujiandaa na mechi dhidi ya Algeria itakayochezwa baadaye mwezi ujao.

Kiungo wa Yanga, Jonas Mkude, naye amerejeshwa katika kikosi hicho cha Kocha Mkuu, Adel Amrouche.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 02/09/2023 | 19:30 | Brighton & Hove Albion vs Newcastle United | 2.50 | 3.55 | 2.50 |
| 02. 02/09/2023 | 19:45 | Go Ahead Eagles vs SC Heerenveen | 2.60 | 3.60 | 2.39 |
| 03. 02/09/2023 | 20:00 | Portimonense SC vs Estrela Amadora | 2.60 | 3.15 | 2.65 |
| 04. 03/09/2023 | 14:00 | Glasgow Rangers vs Celtic Glasgow | 2.36 | 3.45 | 2.75 |
| 05. 03/09/2023 | 14:30 | KAA Gent vs Club Brugge | 2.32 | 3.55 | 2.70 |
| 06. 03/09/2023 | 15:00 | FC Andorra vs Tenerife CD | 2.19 | 3.00 | 3.45 |
| 07. 03/09/2023 | 16:00 | Kalmar FF vs Mjallby AIF | 2.25 | 3.00 | 2.90 |
| 08. 03/09/2023 | 17:00 | Union Saint-Gilloise vs Royal Antwerp FC | 2.31 | 3.35 | 2.85 |
| 09. 03/09/2023 | 17:15 | RCD Mallorca vs Athletic Bilbao | 3.00 | 3.00 | 2.40 |
| 10. 03/09/2023 | 17:30 | GD Chaves vs Moreirense FC | 2.29 | 3.20 | 3.05 |
| 11. 03/09/2023 | 17:30 | Estoril Praia vs Boavista Porto | 2.38 | 3.20 | 2.90 |
| 12. 03/09/2023 | 17:30 | FC Basel 1893 vs FC Zurich | 2.55 | 3.35 | 2.33 |
| 13. 03/09/2023 | 18:00 | Stroemsgodset IF vs Stabaek IF | 2.15 | 3.35 | 2.80 |
| 14. 03/09/2023 | 18:30 | IFK Norrkoping FK vs Djurgardens IF | 2.65 | 3.30 | 2.29 |
| 15. 03/09/2023 | 18:30 | Union Berlin vs RB Leipzig | 3.10 | 3.25 | 2.24 |
| 16. 03/09/2023 | 19:30 | KRC Genk vs RSC Anderlecht | 1.95 | 3.65 | 3.40 |
| 17. 03/09/2023 | 20:15 | Royal Charleroi SC vs St. Truidense VV | 2.17 | 3.35 | 3.10 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## ALHAMISI - 31/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2016 | GKS Katowice W vs Gornik Leczna W | 2.06 | 3.72 | 2.90 |
| 14:35 | 1593 | Nantong Zhiyun vs Qingdao Hainiu | 2.25 | 3.36 | 2.80 |
| 14:35 | 3462 | Beijing Guoan vs Shandong Luneng | 2.34 | 3.40 | 2.64 |
| 16:00 | 5106 | Singida BS FC vs Kitayosce FC | 1.44 | 4.05 | 6.71 |
| 17:00 | 3596 | Al Wasl Dubai vs Hatta Club | 1.57 | 4.16 | 4.47 |
| 17:00 | 4146 | Neftchi Fargona vs FC Andijon | 1.56 | 3.48 | 5.45 |
| 17:00 | 4882 | Shirak Gyumri vs Alashkert Martuni | 4.68 | 3.62 | 1.64 |
| 18:00 | 4122 | Riteriai B vs FK Minija | 2.05 | 3.15 | 3.20 |
| 19:00 | 2486 | Bodo Glimt vs Sepsi Osk | 1.24 | 6.01 | 9.22 |
| 19:00 | 3075 | HJK Helsinki vs Farul Constanta | 2.27 | 3.39 | 2.89 |
| 19:00 | 4137 | Karabakh vs Olimpija Ljubljana | 1.69 | 3.64 | 4.69 |
| 19:00 | 5095 | Artsakh vs Ararat Yerevan | 3.25 | 3.14 | 2.11 |
| 19:30 | 1283 | Baniyas vs Jazira Abu Dhabi | 2.65 | 3.70 | 2.13 |
| 19:30 | 1936 | AL Khaleej Khor Fakkan vs Ittihad Kalba | 2.35 | 3.62 | 2.51 |
| 19:45 | 5377 | Breidablik vs FC Struga Trim Lum | 1.86 | 3.55 | 3.85 |
| 20:00 | 1193 | Sheriff Tiraspol vs KI Klaksvik | 1.44 | 4.29 | 6.59 |
| 20:00 | 1217 | Apoel Nicosia vs KAA Gent | 2.95 | 3.35 | 2.26 |
| 20:00 | 2054 | Sparta Prague vs Dinamo Zagreb | 1.88 | 3.60 | 3.70 |
| 20:00 | 2146 | Brann vs AZ Alkmaar | 3.20 | 3.66 | 2.02 |
| 20:00 | 2283 | Viktoria Plzen vs Tobol Kostanay | 1.23 | 6.00 | 10.00 |
| 20:00 | 2683 | VSG Altglienicke vs Erfurt | 3.21 | 3.51 | 1.99 |
| 20:00 | 2904 | Madla vs Staal Jorpeland | 1.84 | 4.10 | 3.00 |
| 20:00 | 2919 | Tofta Itrottarfelag B68 vs TB Tvoroyri | 1.63 | 3.69 | 4.45 |
| 20:00 | 3009 | Zorya Lugansk vs Slavia Prague | 6.62 | 4.41 | 1.42 |
| 20:00 | 4960 | Aris Limassol vs Slovan Bratislava | 1.83 | 3.51 | 4.01 |
| 20:00 | 5800 | Twente vs Fenerbahce | 2.20 | 3.64 | 2.84 |
| 20:30 | 5290 | PAOK vs Hearts | 1.41 | 4.49 | 6.79 |
| 20:30 | 5346 | 07 Vestur Sorvagur vs EB/Streymur | 1.67 | 3.73 | 4.14 |
| 21:00 | 1181 | Sampaio Correa MA vs Porto Velho EC RO U20 | 1.52 | 4.17 | 4.99 |
| 21:00 | 1321 | Partizani Tirana vs Astana | 3.11 | 3.36 | 2.17 |
| 21:00 | 2724 | Fiorentina vs Rapid Vienna | 1.15 | 7.03 | 14.05 |
| 21:00 | 2976 | Cukaricki St vs Olympiakos | 5.19 | 3.94 | 1.58 |
| 21:00 | 3320 | Ajax vs Ludogorets Razgrad | 1.24 | 6.01 | 9.22 |
| 21:00 | 3373 | BATE Borisov vs KF Ballkani | 3.19 | 3.59 | 2.05 |
| 21:00 | 4314 | Ferencvaros TC vs Zalgiris | 1.28 | 5.58 | 8.57 |
| 21:00 | 4436 | Besiktas vs Dynamo Kiev | 1.51 | 4.14 | 5.65 |
| 21:00 | 4528 | SC Dnipro 1 vs Spartak Trnava | 2.54 | 3.24 | 2.64 |
| 21:00 | 5733 | NK Celje vs Maccabi Tel Aviv | 3.69 | 3.54 | 1.90 |
| 21:00 | 5777 | Adana Demirspor vs Racing Genk | 2.32 | 3.59 | 2.69 |
| 21:15 | 1311 | HNK Rijeka vs Lille | 3.91 | 3.56 | 1.84 |
| 21:30 | 2621 | Eintracht Frankfurt vs Levski Sofia | 1.26 | 5.44 | 9.97 |
| 21:30 | 3908 | FC Lugano vs Union Saint Gilloise | 2.71 | 3.31 | 2.44 |
| 21:30 | 4503 | Brugge vs Osasuna | 2.09 | 3.35 | 3.30 |
| 21:45 | 1569 | Aberdeen vs BK Hacken | 2.54 | 3.43 | 2.54 |
| 22:00 | 1284 | Aston Villa vs Hibernian | 1.16 | 6.81 | 13.96 |
| 22:00 | 1310 | Millonarios FC vs Alianza Petrolera | 1.49 | 3.77 | 6.12 |
| 22:00 | 1550 | Partizan vs Nordsjalland | 2.75 | 3.40 | 2.36 |
| 22:00 | 1809 | Cucuta Deportivo vs Independiente Medellin | 2.96 | 3.11 | 2.27 |
| 22:00 | 4224 | Legia Warszawa vs Midtjylland | 1.92 | 3.55 | 3.60 |
| 22:00 | 5908 | Zrinjski Mostar vs LASK Linz | 2.85 | 3.25 | 2.38 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Alhamisi Agosti 31, 2023

Nipashe




## Man United wajitosa kumsajili Cucurella

UKURASA 21





Mabingwa wapya wa michuano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati kwa Wanawake (CECAFA 2023), JKT Queens ya Tanzania baada ya kuwafunga CBE ya Ethiopia penalti 5-4 katika mechi ya fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa FTC Njeru ulioko Jinja, Uganda jana. **PICHA: MTANDAO**

# MAKALI YA YANGA NI KIPINDI CHA PILI

## ●●●Imefunga mabao 12 kati ya 17 katika muda huo kwenye mechi nne...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi akitamba kwa sasa mchezaji yoyote kwenye kikosi chake anaweza kufunga mabao, timu hiyo inaonyesha makali zaidi katika kipindi cha pili cha kila mechi, imefahamika.

Yanga iliendelea kutoa vichapo katika Ligi Kuu Bara baada ya kuichapa JKT Tanzania mabao 5-0 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi usiku, wafungaji wakiwa ni Stephenie Aziz Ki, Kennedy Musonda, Kouassi Yao na Maxi Nzengeli aliyepachika mawili.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara wanaonekana bora zaidi katika kipindi cha pili, rekodi inaonyesha wamepachika wavuni mabao 12 kati ya 17 kwenye kipindi hicho ndani ya michezo minne iliyocheza mpaka sasa.

Ushindi wa mabao 5-0 walioupata ilipocheza dhidi ya JKT Tanzania katika mechi ya Ligi Kuu Bara juzi usiku, imekamilisha idadi ya mabao nane kati ya 10 ya kipindi cha pili katika mechi zake mbili za Ligi Kuu Bara.

Kwa mujibu wa dawati la takwimu la Nipashe, Yanga imecheza mechi nne mbili za Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Ali Sabieh ASAS na mbili za Ligi Kuu dhidi ya KMC na JKT Tanzania, imefunga jumla ya mabao 17, lakini mabao 12 yakiwekwa kimiani katika kipindi cha pili.

Katika mechi za Ligi Kuu ni mabao mawili tu kati ya 10 ambayo yamefungwa kipindi cha kwanza, ambayo yamefungwa na Dickon Job dakika ya 16 kwenye mechi dhidi ya KMC ikimaliza kwa ushindi wa magoli 5-0, na juzi la Stephane Aziz Ki dakika ya 45 dhidi ya JKT Tanzania.

Mabao manne katika kila mechi yalifungwa kipindi cha pili, Aziz Ki akifunga dakika ya 58, Hafiz Konkoni (69), Mudathir Yahya (75) na Pacome Zouzoua (80) katika mechi dhidi ya KMC, na Kennedy Musonda (54), Yao Kouassi (64), na Maxi Nzengeli (79) na 88 katika mchezo dhidi ya JKT Tanzania.

Mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika hat-

INAENDELEA UK. 23

## Simba yajipanga, Bocco, Mkude warejeshwa Stars

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Robert Oliveira 'Robertinho' amesema mechi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos ya Zambia itakuwa ya kuvutia kwa sababu timu hizo mbili tayari zinafahamiana.

Simba iliwaalika Power Dynamos katika Tamasha la Simba Day lililofanyika Agosti 6, mwaka huu ikiwa ni siku chache kabla ya kukutana kubaini wanaweza kukutana kwenye mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Power Dynamos, mabingwa wa Ligi Kuu Zambia, walisonga mbele katika michuano hiyo inayofanyika kila mwaka baada ya kuwaondoa African Stars ya Namibia.

Robertinho aliliambia gazeti hili ratiba hiyo ameifurahia na hana presha yeyote kuelekea mchezo huo utakaochezwa kati ya Septemba 15 na 17, mwaka huu jijini Lusaka na baadaye kurudiana hapa nchini.

Kocha huyo alisema amejiandaa kukutana na ushindani katika mechi zote mbili kwa sababu kila upande utahitaji kuonyesha ubora wake na hatimaye kutinga hatua ya makundi.

"Sina presha na mchezo wetu wa Ligi ya Mabingwa, nilijiandaa kukutana na timu yoyote msimu huu, hesabu zangu sio tu kutaka kuwang'oa Dynamos, bali ni kuwafunga kwao kabla ya kuja kumalizana nao katika mchezo wa marudiano," alisema Gamondi.

Aliongeza anatarajia wachezaji wake wote watashiriki katika programu za mazoezi kuelekea michuano hiyo baada ya nyota waliokuwa majeruhi, Henock Inonga na Aubin Kramo, afya zao kuimarika na wako tayari kujiunga na wenzao.

"Tuna kikosi imara sana, kitu muhimu ambacho ninafurahia ni kubakiwa na msingi wa timu yangu ya msimu uliopita, hii ni muhimu sana kwa sasa, halafu ukiongeza na hawa wapya, sina wasiwasi na timu yoyote.

Tunawaheshimu Power Dyna-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042